NOVEMBA MMXXIV-TOLEO LA XXXVIII

# NGURUMO
*ya mwandishi*



## Heri ya Krismasi na Mwaka Mpya

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Heri ya Krismasi na Mwaka mpya —Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Sadiki Salum Ng'itu — Uk 03

**New In Town: —** MKATAA PEMA na JUMBA BOVU— uk 04

**PITIO LA VITABU**— BIMA YA PENZI '3'—Uk 06

**MAKALA — SAIKOLOJIA**: Ufanye nini upatwapo na hasira—Uk 06 na 07

**MAKALA:** Mjue WOLE SOYINKA **—** uk 08

**MIAMBA WA AFRIKA:** PATRICE LUMUMBA '2'— Uk 10

**Sako kwa Bako–** Mwl. Juliana Isondo **—**Uk 11

**RIWAYA:** — SHAJARA YA MUUAJI '9'—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7 '20'**-** Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Alibaba na Wezi 40 '15'- Uk 16

**HABARI:** TET yazindua vitabu vya ushindi – Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** Maajabu ya shelf ya vitabu—Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** The Richest Man In Babylon—Uk 19

**MATANGAZO: -** Uk 20

**MALENGA WA KILEO:** Kuna nini Kariakoo? Nimuoe ama nimwache? — Uk 21

**HABARI PICHA: -** Uk 22

**KUTOKA MAKTABA:** Maisha ni Mapambano '5'-Uk 23

**ELIMU JAMII:** — Hakuna Mwanafunzi Anayependa Kufeli —Uk 24

**HADITHI:** — Happy New Year Uk. 26—27 na SHEMEJI USIZIME TAA…!

## TAHARIRI:

### HERI YA KRISMASI NA MWAKA MPYA

Wasalaam,

Tukiwa mbioni kuumaliza mwaka huu wa 2024, ni matumaini yangu nyote mu wazima na bukheri wa afya.

Tunapoumaliza mwaka huu hatuna budi kumshukuru Mungu kwa mema yake. Maana mimi na wewe tuna nini hata mpaka leo hii atupendelee pumzi yake? Ni wangapi wamerudi kwake ndani ya mwaka huu?

Sema asante Mungu! Kumbuka kutoa sadaka ya shukrani na omba neema kwa mwaka unaokuja kwako na kwa familia yako bila kuwasahau wote wanaokuzunguka.

Katika mwezi wa Novemba tumepoteza makumi ya ndugu zetu katika mporomoko wa ghorofa pale Kariakoo. Hakuna aliyependa kufa kifo kama kile lakini wakati mwingine ni ngumu kuelewa apangalo Mola.

Niseme nini basi? Tuendelee kujifunza na kuishi mapenzi ya Mwenyezi Mungu kila wakati hasa tunapoelekea sikukuu hizi mbili kubwa; Krisimasi na Mwaka mpya. Lakini pia tukumbuke kubana matumizi kwani Januari ya ada imegonga hodi.

Sisi timu nzima ya Ngurumo tunakutakieni sikukuu njema sana. Na Mungu awe nanyi. Tutaonana Januari 2025.

***Richard Mwambe***
***CEO—Jamvi la Simulizi***

**NGURUMO YA MWANDISHI**


**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## MWANDISHI WETU:
## SADIKI SALUM NG'ITU

**Moja kwa moja mpaka kijijini Nandagala, wilayani Rwangwa, mkoani Lindi.**

**Tunamrejelea mwandishi Sadiki Ng'itu anayefanya vizuri kwenye mtandao pendwa wa Facebook na riwaya zake mbalimbali.**

**Ni andiko tulilowahi kulichapa huko siku za nyuma...**



Na Mwandishi wetu
Jina langu ni SADIKI SALUMU NG'ITU, Nimezaliwa mkoani Lindi. Ni mtoto wa nne katika familia yenye watoto watano. Nimewahi kuishi Musoma kwa muda wa miaka saba. Nimefanikiwa kusoma hadi kidato cha nne. Pia nina Certificate ya RECORDS MANAGEMENT.
Napatikana Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Ruangwa kijijini Nandagala.

Uandishi nimeanza rasmi mwaka 2019. Nikisema rasmi namaanisha kuanza kupost mitandaoni.
Jinsi nilivyoanza uandishi rasmi, nakumbuka kuna mtu mmoja alikuwa anapost kwenye group, jina alilokuwa akitumia sina kumbukumbu nalo sana. Na hiki ni kitu kinachoniumiza, maana bila yeye nisingefahamika kwa sasa.
Nahisi kama alikuwa anajiita Emmanuel ila nimesahau jina la ubini wake.. Yeye ndiye aliweka post kwa ambaye anajihisi ana kipaji, basi anampa nafasi ya kupost. Kwa atayepata likes nyingi atapewa nafasi jumla. Hapo ndipo nilianza kwa kuandika riwaya yangu ya kwanza kabisa, FIGHT UNTILL DEATH (F U D).

Kilichonisukuma kuwa mwandishi;
Mapenzi yangu makubwa na kusoma maandishi ya wengine. Mapenzi ambayo nilijengewa na marehemu Baba yangu. Baada ya kusoma sana, na kujitambua kuwa ninaweza kufanya kitu fulani, nikapata ujasiri wa kuanza kuandika ili wengine wasome.

Ni ngumu sana kwangu kusema nani namkubali sana yaani gumu sana hili. Kwakuwa nimeulizwa mmoja, ila angalau mungetaka wawili.
Okey, ni George Iron Mosenya Mwalimu wangu. Napenda kumuita hivyo. Huyu ndiye mtu ninayehusudu zaidi maandishi yake.

Hadi sasa nimeandika vitabu 19. Kama ifuatavyo.
Orodha ni;
1. FIGHT UNTILL DEATH
2. TATTOO YA MUUAJI
3. KITANZI
4. KIVULI (Toa mguu, niweke mguu)
5. AISEEE! (Lazima Ukae)
6. PURUKUSHANI
7. PURUKUSHANI 2 (Liwalo na liwe)
8. CHUMBA CHA MAUAJI
9. ADELINA (Apatikane, hai au mfu)
10. PLATE NUMBER
11. UTAZIKA AU UTASAFIRISHA?
12. MATUKUTA (Lielewe jina langu)
13. SHINIKIZO (Navuka mstari, naifuata hatari)
14. SHINIKIZO 2 (Ndani ya Mjengo)
15. HUKUMU YA HAKIMU
16. NIITE MJEDA
17. WARAKA ULIOSAHAULIKA
18. PENZI LANGU UHAMISHONI
19. HESABU ZA MUUAJI (Hii ndio inayoendelea gazetini.)

Faida ya kwanza ni faraja ya moyo. Kuandika kwenyewe ni furaha kwangu, kusomwa ni faraja ya pili.
Pia faida nyingine ni kujuana na watu ambao sikuwahi kutegemea kujuana nao (Waliopo kwenye Mfumo- Haswa Usalama wa Taifa)

Wapenzi wa kazi zangu, nawashukuru kwa kunichagua kuwa mwandishi wao. Waandishi tupo wengi, hivyo kuwa moja ya wanaowafurahia nawashukuru sana.
Nawaomba waendelee kuniamini, pia nawaahidi sitawaangusha.
Kwa atayehitaji kazi zangu, zinapatikana kwenye ukurasa wangu wa Facebook, SN Hadithi
Pia kwa mawasiliano ya simu 0789243142 (WhatsApp pia.) au kwa namba 0755496264.

*Sadiki Salumu Ng'itu*

## NEW IN TOWN :
## MKATAA PEMA na JUMBA BOVU

**MKATAA PEMA—Dkt. Rose Mbijima**


KABLA ya ujio wa wakoloni barani Afrika, ngano zilitzamwa kama shuke mahsusi iliyohifadhi hekima na falssa za jamii mbalimbali. Katika nyakati hizi ambazo sayansi na teknolojia inatishia kuua ngano na fasihi simulizi kwa jumla, jitihada za makusudi zinatakiwa kufanywa kunusuru hali hiyo. Kitabu hiki ni mojawapo ya jitihada hizo.

Ngano zilizomo kwenye kitabu hiki zinaturudisha miaka mingi nyuma ambapo fasihi simulizi, ngano ikiwemo, ilikuwa siyo tu muhimu bali mfumo wa elimu jadi uliotumika kutoa mafunzo muhimu kwa jamii hasa kwa watoto na vijana. Hata sasa fasihi simulizi ni muhimu kwa jamii, kwani inatoa mafunzo yanayohitajika katika jamii. Hivyo, sio sahihi kudhani kwamba ngano zimepitwa na wakati katika jamii zetu zenye mfumo changamani wa maisha. Maendeleo ya kidijitali yanatakiwa kusaidia kuzipa sura mpya ngano za Kiswahili na siyo kuziua.

Kitabu kimesheheni ngano nyingi zenye mafunzo si haba yaliyobebwa na fani murua, kinaweza kusomwa na wanafunzi na walimu wa fasihi simulizi, wa viwango mbalimbali Afrika Mashariki na hata Afrika kwa ujumla.

Kitabu hiki kinapatikana kwenye

- **Duka la Vitabu la Kona ya Riwaya Kinondoni, Simu 0655428085**
- **Mwandishi 0688851445**




**JUMBA BOVU— XAVERY LUOGA**

KATIKA mitaa yenye giza la matumaini yaliyopotea, Clara na Tina, wakiwa wahanga wa maisha ya hatari ya kujiuza mwili, wanajikuta wakitumbukia kwenye mtego mbaya uliotegwa na Mr. Maziba.

Baada ya Clara kuiba begi alilodhani lina pesa nyingi, kumbe ni mzigo mzito aliouchukua hatari kupita maelezo.

Sasa, akiwa shikinizoni, anapokea simu kutoka kwa Mr maziba, ya kumwamuru afanikishe huo mzigo kumfikia mtu mwingine, Benson.


Benson, mwanaume aliyewahi kuacha alama isiyofutika kwenye maisha ya Ckara, katika safari ya mapenzi yao yenye misukosuko.

Lakini jea, anaweza kuepuka mtego ya uhalifu angali Inspekta Patti na kikosi chake wameshawaka moto kufuatilia kila mshono wa sakata hili. Na katika mchezo huu wa paka na panya, maswali mazito yanabaki: nani ataangukiwa na jumba bovu? Clara, Benson, Inspekta Patti au Mzee Maziba?

Jumba Bovu ni hadithi ya vuta nikuvute, yenye uhalisia wa maisha, mapenzi na hatari zinazoweza kumwangusha yeyote aliyeshindwa kuchagua njia sahihi.

Kitabu hiki kinapatikana

- **Duka la Kona ya Riwaya Kinondoni. Aimu namba 0655428805**
- **Mwandishi 0672493994**



## PITIO LA VITABU




# KITABU: BIMA YA PENZI—03

***Inatoka toleo lililopita…***

Mapenzi yamekua chanzo cha vichaa wengi mitaani, mapenzi yamekua chanzo cha watu kuumizana akili na hisia.Wakati fulani niliwahi kuwaza, hili neno "NAKUPENDA" kwanini lisitafutiwe mbadala mwingine wa neno, kwamba kwanini mwanaume asimwambie mwanamke "nimekutamani",na kwamba ibaki kuwa ni chaguo la mwanamke kukubali kutamaniwa. Na kuwa, kama amekubali kutamaniwa basi atoe masharti yake ya kushiriki mahusiano kulingana na kutamaniwa? Kwamba "Zubeda, mi nimekutamani" na Zubeda nae akubali au akatae kutamaniwa, na akikubali aseme "John, ili kukidhi matamanio yako nilipe kiasi kadhaa" na John nae aridhie kulipia kuliko kufanya matumizi mabaya ya neno "nakupenda".

Yaani unamuona tuu Neema mtandaoni eti unamwambia unampenda, *bro, are you serious?* Unajua kupenda wewe? Hili neno linanikumbusha wakati shemeji na kaka yenu ananitongoza, na hapo ilikua ananiona macho kwa macho kila iitwapo jioni. Alikua ameshayaona hayo macho mnayonisimangia kila wakati, ameshauona huo uumbaji wa Mungu kwa jinsi mwili ulivyojengeka, bado pamoja na kuniona,aliponambia eti "Nakupenda" nilimkatalia, nikamwambia "wewe haujanipenda, ila umenitamani". Jamaa akaona hapa hiki kisiki, na ashukuru Mungu watoto ndio waliofanya niwe nae. Mpaka leo tumeshakata miaka 14 pamoja. Sema Mashaalaahh.

Mapenzi yanaumiza sana, mwanzo huanza vizuri, vicheko, furaha, bashasha. Mkishazoeana mambo yote hupotea. Inaanza kejeli, matusi, kudharauliana, kuchokana, kusalitiana na mbaya zaidi siku hizi watu wameboresha ukatili unakuta ghafra tuu UMEACHWA BILA SABABU, yaani ghafra tu kimya. Mlikua mkichart mara umekaliwa kimya, bila sababu umenuniwa, jamani, mnatupa kazi washauri kumshauri huyu mtu mpaka akae sawa kwa tamaa zako za muda mfupi,we umemtamani basi sema "nimekutamani". Mwambie kabisa kuwa unataka mcheze, sio kusema unampenda ilihali wewe unataka kupita tu.

Sasa hivi watu wanaenda mbali zaidi, kwa kitu kinachoitwa wivu uliopindukia, watu wanaua wapenzi wao, watu wanajiua wao wenyewe. Jamani, hakuna nafsi imekuja kutawala nafasi nyingine, UKIONA YANASHINDIKANA MWACHE AENDE, MSUBIRI WA KWAKO AMBAE HAMTOSUMBUANA. Sasa kwanini umuue? Kwanini ujiue? Wengine walivyo wapuuzi na katili kabisa wanaua hadi watoto, tunaenda wapi? Ni kweli kwamba huyo mwanamke au mwanaume yeye ndiye anaeyajua mapenzi peke yake? Ni kweli kwamba akikuacha hupati mwingine? Ni nini tunafanya wanadamu, kwamba huwezi kumuacha AENDE? Kwamba yeye huyo ndio peke yake ulimwengu mzima?. Tubadili fikra zetu wapendwa, ukiona yameshindikana MWACHE AENDE. Usimfanyie ukatili, kumbuka kuwa ukiona hamuelewani na umejaribu njia zote za kumrekebisha umeshindwa basi jua huyo sio wako, MWACHE AENDE, Mungu atakupa aliye bora kuliko huyo. USIMUUE WALA USIJIUE.

Wacha niishie hapa kwa leo, nadhani umenielewa,.

Sasa Kitabu BIMA YA PENZI kinapatikana nchi nzima,kwa Dodoma unaweza kufika dukani kwa. AZIZ BOOK STORE, lililopo barabara ya sita nyuma ya bank ya NMB au katika duka la CAPITAL BOOK STORE, lililopo barabara ya sita, karibu na NYERERE SQUARE. Au nipigie kupitia simu +255 763 013 206 nikurahisishie kukipata kwa uhakika kabisa,hata uliyepo mkoani nitakutumia pindi ukamilishapo malipo na gharama ya usafiri.

Au wasiliana na mwandishi wa kitabu hiki moja kwa moja kupitia simu no. +255 657 532 334.

Bei ya kitabu ni rafiki kabisa, tofauti na elimu iliyopo ndani. Kwa sh. 25,000/= tuu unapata elimu kubwa saana.

Wako katika uchambuzi,.

***The Magic Author,***

***Madame Neema Mgao,***

# -SAIKOLOJIA-

## UFANYE NINI UPATWAPO NA HASIRA?

**The Magic Author,**

**Madame Neema Mgao.**



**UFANYE NINI UPATWAPO NA HASIRA?**

Habari yako ndugu yangu, sina shaka unaendelea vizuri na majukumu yako ya kila siku. Karibu katika kuisoma makala hii ya Saikolojia kwa mwezi huu wa Novemba. Ikiwa umezongwa na mitihani miwili mitatu nikusihi tu uweze kuwa na subira katika utatuzi wa mambo hayo yakuzongayo.

Aidha, nitumie ukurasa huu kuwapa pole wale wote waliokumbwa na janga la kuporomokewa na jengo katika soko la KARIAKOO. Natambua hasara kubwa waliyoipata wafanyabiashara katika jengo husika. Hasara ya mali, na jengo pia. Kwa sababu ambazo pengine zilizoshindwa kuepukika au zilizoweza kuepukika (MUNGU NDIE AJUAE) na zisilete hasara kwa watu na kwa taifa kwa ujumla. Taifa limepoteza nguvu kazi kutokana na vifo vilivyotokea, ndugu wamepoteza wapendwa wao, kuna watoto wamepoteza wazazi wao, kiuhalisia ni janga lililotikisa sio tu taifa la Tanzania lakini pia Africa na dunia kwa ujumla.

Lakini kile nilikiona, ni upendo mkubwa na mshikamano katikati ya Watanzania katika uokoaji kuhakikisha walionaswa na kifusi wanatoka wakiwa salama au miili yao kupatikana. Niliona ushirikiano kati ya jeshi la uokoaji na watu wote waliokuwepo katika eneo husika. ROHO ZA MAREHEMU ZIPATE REHEMA KWA MUNGU, ZIPUMZIKE KWA AMANI, AMINA. Poleni KARIAKOO, MTASIMAMA TENA.

**UFANYE NINI KUJITULIZA UPATWAPO NA HASIRA?**

**HASIRA NI NINI?**

Hasira ni mhemko hasi utokao ndani ya akili ya mtu pale asababishiwapo maumivu au fikra zinapojeruhiwa pale afanyiwapo jambo tofauti na matarajio au matakwa yake.

**VISABABISHI AU VICHOCHEZI VYA HASIRA NI VIPI?**

Hasira huweza kuchochewa na mambo mengi sana kulingana na mazingira husika. Hasira hukaa kwa mtu yule asiye na uwezo wa kujizuia kukasirika, asiyeweza kutawala hisia zake. Vipo visababishi vingi ambavyo vinaweza kusababisha mtu kukasirika. Tuone yale maeneo nyeti ambayo yanaweza kumsababishia mtu kuibua hisia yake ya chuki au hasira.

**A] MAHUSIANO/ NDOA.**

Eneo la mahusiano na ndoa hivi sasa limekua likiongoza katika kuchochea au uchochezi na usababishwaji wa wenza kuwa na hisia hasi au hasira. Kwa namna moja au nyingine tumeshuhudia dunia ikishuhudia matukio mengi ya kikatili ambayo wana ndoa au walio kwenye mahusiano wakitendeana ukatili ambao hupelekea madhara kimwili na kihisia katika maisha ya mahusiano yao.

**B] MAENEO YA KAZI/ BIASHARA**

Maeneo ya kutafutia riziki yanaweza pia kuwa mahali ambapo chuki au hasira hutawala au kupatikana pia.Maeneo ya kazi au katika biashara yanaingia moja kwa moja kama maeneo yanayoweza kusababisha hasira kuzalishwa.

**C] MIJADALA YA KUNDI SOGOZI.**

Kundi sogozi/group la whatsApp lisipotumiwa ipasavyo huweza kusababisha au kuibua chuki baina ya watu na watu au mtu na mtu. Wapo watu ambao huweza kuzalisha  hasira kwa mwingine kulingana na mada mbalimbali jadiliwa katika nyakati husika. Kama una moyo mdogo ni vyema usishiriki katika majibizano ya kundi mahalia.

Yapo maeneo au vitu vingi ambapo hasira huweza kusababishiwa katika maeneo husika. Nimeona katika toleo hili tuone japo kwa uchache tuu maeneo hayo.

# -SAIKOLOJIA-

## UFANYE NINI UPATWAPO NA HASIRA?

**UFANYE NINI KUJITULIZA UPATWAPO NA HASIRA?**

Zipo njia nyingi za kufuata au za kufanya ili kujituliza wakati upatwapo na hasira.

Lakini unadhani kwanini nasema ujitulize?

Tabibu mkubwa wa kuishusha hasira yako ni wewe mwenyewe. Mwenye uwezo wa kukutuliza pale ukasirikapo ni wewe mwenyewe. Hata kama mtu mwingine akatoka atokapo na kuja kukutuliza, kama haujaamua wewe mwenyewe kushuka na kusikiliza basi huwezi kutuliza hizo hasira. Kumbe mtu pekee anaweza kutuliza munkari wa hasira zako ni wewe mwenyewe.

Fanya mambo haya kujituliza uwapo na hasira.

**JIFUNZE KUTAWALA HISIA ZAKO**

Moja kati ya zoezi gumu kabisa ni zoezi la kutawala hisia zako. Kitaalamu, mwanaume anaongozwa na matamanio halafu hisia hufuata baadae, huku mwanamke yeye huongozwa na hisia kisha matamanio au kupenda hufuata baadae. Ndio maana  mwanaume anapomhitaji mwanamke anawasilisha matamanio yake, lengo ni ili apate kutimiziwa matamanio yake, huku mwanamke anapokubali kupokea yale matamanio, yeye huzalisha hisia juu ya mwanaume yule. Ndio maana wanasema “mwanamke akipenda, amependa kweli”. Wapo sahihi ,kwasababu mwanamke kwanza anaongozwa na hisia halafu kupenda ndio kunafwata.

Tuachane na hisia hizo, nazungumzia uwe na uwezo wa kutawala hisia zako. Tawala hizo hisia zikupazo hasira, hasira hukaa kwa mpumbavu.

**FANYA JAMBO LIKUPALO FURAHA**

Upatapo hasira jitahidi sana kufanya jambo likupalo furaha. Kuna mtu anasema apatwapo na hasira yeye huiondoa hasira hiyo kwa kulima sana. Mwingine anasema apatwapo na hasira yeye husikiliza saana muziki. Yaani fanya jambo lile linalokupa furaha au linalokupa amani.

**ONDOKA KWA MUDA.**

Ondoka kwa muda hapo palipokusababishia hasira, kama ni kazini mmekwazana na wafanyakazi wenzio basi ondoka kwa muda mahali hapo,

Kama mmehitilafiana na mpenzi wako, mume au mke wako ondoka kidogo mahali hapo. Hata kama iwe mmetofautiana kwa mazungumzo ya simu. Hapo ulipokaa muda mnagombana unashauriwa kwa muda mchache  inuka, hama kidogo ili ubadilishe mazingira kidogo ili kubadili kidogo hali ya hewa. Kawaida ya ubongo wa binadamu ukikaa mahali pamoja na kutulia tuu hushindwa kutengeneza picha mpya ili kuleta matokeo chanya au hasi . Ondoka kwa muda mahali hapo ili utengenze picha mpya na ili uweze kufanya kwa upya .

Kwa leo tuishie hapa. Ni Imani yangu kuwa mada hii itakusaidia na matamanio yangu ni kuwa unipe ujumbe wa namna gani mada hii imekujenga kupitia mawasiliano yangu hapa chini. Pia kitabu cha JITIBIE KISAIKOLOJIA bado kipo mtaani, nifuate FB kwa jina la NEEMA MGAO ili kupata taarifa zaidi za namna ya kukipata kitabu hiki.

Wasiliana na mimi ili kupata ushauri wa Kisaikolojia kupitia +255763013206.

Asante.

The Magic Author,

Madame Neema Mgao.

## WOLE SOYINKA
## MWANAFASIHI WA KWANZA MWAFRIKA KUPATA TUZO YA NOBEL

***Kutoka toleo lililopita…***

Mnamo 1970, alitayarisha tamthilia ya 'Kongi's Harvest', pia tamthiliya hiyo ikaigizwa kama filamu. Mwaka huo huo, alichapisha tamthiliya ya *'Madmen and Specialists'*. Wole Soyinka pamoja na kikundi cha waigizaji 15 wa Kampuni ya Sanaa za maonesho cha Chuo Kikuu cha Ibadan, walifunga safari kwenda Marekani, hadi Kituo cha Eugene O'Neill Memorial huko Waterford, Connecticut, ambapo walihusika kutayarisha tamthiliya zake na kuzionesha kwenye majumba ya maonesho.

Pia, suala hilo Iiliwapa wote (Wole Soyinka na vijana 15) uzoefu wa utayarishaji wa maonyesho katika nchi zingine zinazozungumza Kiingereza. Mnamo 1971, mkusanyiko wake wa mashairi *'A Shuttle in the Crypt'* ulichapishwa. Pia, tamthiliya yake ya 'Madmen and Specialists' ilisimamiwa na kutolewa na chuo kikuu cha Ibadan mwaka huo. Wole Soyinka alisafiri hadi Paris kuchukua nafasi ya kiongozi kama Patrice Lumumba (kuigiza kama Patrice Lumumba), Waziri Mkuu wa kwanza aliyeuawa wa Jamhuri ya Kongo, katika uandaaji wa tamthiliya ya *'Murderous Angels'* ya Conor Cruise O'Brien iliyokuwa inahusu machafuko ya kisiasa ya nchini Congo.

Mnamo Aprili 1971, akiwa na wasiwasi kuhusu hali ya kisiasa nchini Nigeria, Soyinka alijiuzulu wadhifa wake katika Chuo Kikuu cha Ibadan. Mnamo Julai 1971 jijini Paris, sehemu za tamthilia yake maarufu ya *'The Dance of The Forests'* zilitayarishwa na kuchezwa katika matamasha.

Mnamo 1972, riwaya yake ya *'Season of Anomy'* na mkusanyiko wa tamthiliya zake zote zilichapishwa na Oxford University Press. Kitabu chake maarufu cha '*The Man Died*', kinachohusu matukio mengi aliyopitia alipokuwa gerezani kilichapishwa pia mwaka huo. Alitunukiwa shahada ya udaktari ya Honoris Causa na Chuo Kikuu cha Leeds mwaka wa 1973.

Katika mwaka huo huo Jumba la Kuigiza la Kitaifa, London, lilianzisha na kurusha tamthilia ya '*The Bacchae of Euripides*', na tamthilia zake za '*Camwood on the Leaves'* na '*Jero's Metamorphosis'* pia zilichapishwa kwa mara ya kwanza .Kazi zake nyingi zilitumika kufundishia katika vyuo vingi barani ulaya la Amerika. Kuanzia mwaka wa 1973 hadi 1975, Wole Soyinka alitumia muda katika masomo ya kisayansi.
Mnamo 1974, mkusanyiko wa tamthiliya zake, toleo la II ilitolewa na Oxford University Press. Mnamo 1975 Soyinka alipandishwa cheo na kuwa mhariri wa *Transition,* gazeti lililokuwa na makao yake katika mji mkuu wa Ghana wa Accra, ambako alihamia kwa muda. Aliandamana dhidi ya utawala wa kijeshi wa Idi Amin nchini Uganda. Baada ya mabadiliko ya kisiasa nchini Nigeria na kupinduliwa kwa utawala wa kijeshi wa Gowon mwaka wa 1975, Wole Soyinka alirejea katika nchi yake na kuanza tena nafasi yake kama Mwenyekiti wa Fasihi Linganishi katika Chuo Kikuu cha Ife.

Mnamo 1976, alichapisha mkusanyiko wake wa mashairi *'Ogun Abibiman'*, pamoja na mkusanyo wa insha uitwao '*Myth, Literature and the African World'*. Wole Soyinka alichunguza asili ya fasihi ya Afrika na kulinganisha na fasihi za ulaya na maeneo mengine, pia aliandaa miadhara mbalimbali na kuwaalika waandishi na wana fasihi wengi kutoka nchi mbalimbali katika katika Taasisi ya Mafunzo ya Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Ghana ili kujadili na kukuza fasihi ya Afrika. Mnamo Oktoba, toleo la Kifaransa la Ngoma ya Misitu lilichezwa huko Dakar, huku Ife, tamthilia zake za 'Death' na 'The King's Horseman' zilionyeshwa kwa mara ya kwanza.

Mnamo 1979, Wole Soyinka aliongoza na kuigiza tamthilia ya Jon Blair na Norman Fenton ya *'The Biko Inquest',* kazi iliyoelezea maisha ya Steve Biko, mwanafunzi wa Afrika Kusini na mwanaharakati wa haki za binadamu ambaye alipigwa hadi kufa na vikosi vya polisi vya ubaguzi wa rangi. Mnamo 1981, Wole Soyinka alichapisha kazi yake ya Aké: The Years of Childhood (autobiographical work), ambayo ilishinda tuzo ya 1983 ya Anisfield-Wolf Book Award.

Wole Soyinka alianzisha kikundi kingine cha maonyesho kilichoitwa *'Guerrilla Unit'*. Lengo lake lilikuwa kufanya kazi na wananchi na kuchanganua matatizo na kuyaelezea kwenye kazi za fasihi, ilikuwa mbinu ya kufikisha malalamiko na matatizo ya jamii kwa njia ya fasihi. Mna-

mo 1983 tamthilia yake ya *'Requiem for a Futurologist'* ilipata onyesho lake la kwanza katika Chuo Kikuu cha Ife. Ukiachana na tamthiliya na riwaya, Wole Soyinka alitunga nyimbo na zikafanikiwa kupendwa na kutumbuizwa na wasanii wakubwa wa nchi ya Nigeria, moja ya wimbo wake pendwa ni *'I Love You My Country'*. Mnamo 1984, aliongoza filamu ya *'Blues for a Prodiga'* ambayo ilionyeshwa katika Chuo Kikuu cha Ife. Pia, tamthiliya yake ya *'A Play of Giants'* ilitolewa mwaka huo huo.

Miaka ya 1975-84, Wole Soyinka alikuwa akifanya kazi zaidi kisiasa. Katika Chuo Kikuu cha Ife, kazi zake za utawala zilijumuisha usalama wa barabara za umma. Alikosoa ufisadi katika serikali ya Rais aliyechaguliwa kidemokrasia 'Shehu Shagari'. Nafasi ya Wole Soyinka ilichukuliwa na jenerali wa jeshi aliyeitwa Muhammadu Buhari, mara nyingi Wple Soyinka akaanza kutofautiana na jeshi. Mnamo 1984, mahakama ya Nigeria ilipiga marufuku kitabu chake cha *'The Man Died: Prison Notes'*. Lakini, mnamo 1985, tamthilia yake ya *'Requiem for a Futurologist'* ilichapishwa jijini London na Rex Collings.
Wole Soyinka alitunukiwa Tuzo ya Nobel ya Fasihi mwaka wa 1986, na kuwa Mwafrika wa kwanza kushinda tuzo hiyo. Katika hotuba ya Wole Soyinka kipindi anapokea tuzo hiyo alipinga vikali ubaguzi wa rangi uliokuwa ukiendelea Afrika Kusini, pia aliweka wazi kuwa anaunga mkono harakati za Nelson Mandela na chama chake cha kisiasa (ANC) Mwaka huo huo, alipokea tena Tuzo ya fasihi ya Agip.

Mnamo mwaka wa 1988, mkusanyo wa mashairi yake alioupa jina la *'Mandela's Earth'*, ulichapishwa.

Mwaka huo huo, Wole Soyinka alikubali nafasi ya kuwa 'Professor of African Studies and Theatre' katika Chuo Kikuu cha Cornell. Mnamo 1989, alitoa riwaya iliyokuwa inaelezea maisha ya baba yake mzazi, riwaya hiyo iliitwa *Isara: A Voyage Around Essay'*.
Mnamo Julai 1991, BBC African Service ilisambaza tamthiliya yake ya *'A Scourge of Hyacinths'*, mwaka uliofuata (1992) huko Siena (Italia), tamthilia yake ya *'From Zia with Love'* ilianza kuonyeshwa. Kazi zote mbili zinaelezea siasa mbovu na matukio ya hovyo yaliyotokea nchini Nigeria katika miaka ya 1980. Mnamo 1993, Wole Soyinka alitunukiwa udaktari wa heshima (honorary doctorate) kutoka Chuo Kikuu cha Harvard. Mwaka uliofuata, tamthilia yake ya *'The Beatification of Area Boy'* ilichapishwa. Mnamo Oktoba 1994, aliteuliwa kuwa Balozi wa Nia Njema wa UNESCO kwa Ukuzaji wa Utamaduni wa Kiafrika, haki za binadamu, uhuru wa kujieleza, vyombo vya habari na mawasiliano.

Mnamo Novemba 1994, Wole Soyinka alitoroka kutoka Nigeria kupitia mpaka na Benin na kisha kuelekea Marekani baada ya kusumbuliwa na taifa la Nigeria. Mnamo 1997 alishtakiwa kwa uhaini na serikali ya Jenerali Sani Abacha nchini Nigeria kwa kazi zake za kifasihi zinazopinga uonevu, pamoja na harakati zake za kisiasa zenye kuhitaji usawa. Bunge la Kimataifa la Waandishi lilianzishwa ili kutoa msaada kwa waandishi walioathiriwa na wanaoathiriwa na mateso au ukidhani kutoka serikalini. Soyinka alikua rais wa pili wa shirika kuanzia 1997 hadi 2000. Mwaka 1999, tamthilia yake iliyoidhinishwa na BBC iitwayo *'Document of Identity'* ilirushwa hewani na BBC Radio 3, ikisimulia kisa cha kutunga kilichoelezea matatizo yaliyomkumba binti na familia yake walioikimbia Nigeria kuelekea Marekani mwaka 1996.
Tamthilia ya Wole Soyinka *'King Baabu'* ilionyeshwa kwa mara ya kwanza mjini Lagos mwaka wa 2001, iliyoelezea uongozi wa kidikteta katika mataifa ya Afrika.

Mnamo Aprili 2007, Soyinka alitoa wito wa kufutwa kwa uchaguzi wa urais wa Nigeria uliofanyika wiki mbili mapema, uliokumbwa na ulaghai na ghasia. Alipata upinzani mkubwa kutoka serikalini mpaka kuwa na hofu ya maisha yake. Mnamo Agosti 2014, Wole Soyinka alitoa hotuba yake yenye jina *"From Chibok with Love"* chini ya World Humanist Congress huko Oxford, iliyoandaliwa na International Humanist and Ethical Union na British Humanist Association. Mada ilikuwa *'Freedom of thought and expression: Forging a 21st Century Enlightenment'*. Alitunukiwa Tuzo ya Kimataifa ya Kibinadamu ya 2014.
Mnamo Desemba 2020, Soyinka alielezea mwaka wa 2020 kuwa mwaka wenye changamoto nyingi zaidi katika historia ya taifa, akisema: "Kwa msukosuko uliotokea mwaka wa 2020, na jinsi shughuli zinavyopungua, hali imekuwa ya kuchukiza na mbaya sana". Vile vile alielezea namna janga la Korona – 19 lilivyoathiri taifa lake.

Soyinka ameoa mara tatu na talaka mara mbili. Ndoa yake ya kwanza ilikuwa 1958 na marehemu mwandishi wa Uingereza Barbara Dixon, ambaye alikutana naye katika Chuo Kikuu cha Leeds katika miaka ya 1950. Barbara alikuwa mama wa mtoto wake wa kwanza wa kiume, Olaokun, na binti yake Morenike. *Inaendeke uk. Wa 19*

**KATIKA safu yetu ya MIAMBA WA AFRIKA, leo tunakueleta Patrice Lumumba. Huyu alikuwa Waziri Mkuu wa nchi ya Congo DRC. Ni mmoja kati ya waafrika wachache waliokataa kuwa vibaraka wa wakoloni, alipambana kuikombo Congo, lakini nini kilimkuta? Tuendelee...**



**Patrice Lumumba**

***SEHEMU YA 2***

**KIONGOZI WA MNC**

Baada ya kuachiliwa, Lumumba alisaidia kuanzisha chama cha Mouvement National Congolais (MNC) mwaka 1958 na haraka akawa kiongozi wa chama hicho. MNC, tofauti na vyama vingine vya Kongo vilivyokuwa vinakua wakati huo, havikutoa msingi maalum wa kikabila. Ilitangaza jukwaa lililojumuisha uhuru, mchakato wa kudhihirisha Uafrika wa serikali, maendeleo ya kiuchumi yanayoongozwa na serikali, na uasi katika masuala ya kigeni.

Lumumba alikuwa na umaarufu mkubwa miongoni mwa watu na kwa hivyo alikuwa na uhuru zaidi wa kisiasa kuliko wenzake waliokuwa wanategemea uhusiano wa Kibelgiji.

Lumumba alikuwa mmoja wa wawakilishi waliokuwa wakiiwakilisha MNC katika Mkutano wa Watu wa Afrika Wote uliofanyika Accra, Ghana, mwezi Desemba 1958. Katika mkutano huu wa kimataifa, ulioandaliwa na rais wa Ghana, Kwame Nkrumah, Lumumba alithibitisha zaidi sifa zake za pan-Africanism. Nkrumah alikuwa na ushawishi na alivutiwa na akili na uwezo wa Lumumba.

Mwaka 1959, MNC iligawanyika katika MNC-L iliyoongozwa na Lumumba, na MNC-K yenye msimamo mkali na wa shirikisho. Mwisho wa mwezi Oktoba mwaka 1959, Lumumba, akiwa kiongozi wa MNC, alikamatwa kwa kuchochea ghasia za kupinga ukoloni katika Stanleyville ambapo watu 30 waliuawa. Alihukumiwa kifungo cha miezi sita. Tarehe ya kuanza kwa kesi hiyo ya 18 Januari 1960 ilikuwa siku ya kwanza ya Mkutano wa Meza ya duara (mazungumzo) wa Kongo mjini Brussels, ulioandaliwa kupanga mustakabali wa Kongo.

Licha ya kifungo cha Lumumba, MNC ilishinda kwa ushindi mkubwa katika uchaguzi wa mitaa mwezi Desemba nchini Kongo. Kutokana na shinikizo kubwa kutoka kwa wawakilishi waliokuwa na wasiwasi kuhusu kesi ya Lumumba, aliachiliwa na kuruhusiwa kuhudhuria mkutano wa Brussels.

**Uhuru na Uchaguzi kama Waziri Mkuu**

Mkutano huo ulikamilika tarehe 27 Januari 1960 kwa tamko la uhuru wa Kongo. Ulipanga tarehe 30 Juni 1960 kuwa siku ya uhuru, huku uchaguzi wa kitaifa ukifanyika kati ya tarehe 11 hadi 25 Mei 1960. Chama cha MNC kilishinda wingi wa viti katika uchaguzi huo. Wiki sita kabla ya tarehe ya uhuru, Walter Ganshof van der Meersch aliteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Afrika wa Ubelgiji. Aliishi Léopoldville, akawa kwa vitendo waziri mkazi wa Ubelgiji nchini Kongo, akisimamia nchi pamoja na Gavana Mkuu Hendrik Cornelis. Alipewa jukumu la kumshauri Mfalme Baudouin kuhusu uteuzi wa mwezeshaji wa serikali.

Mnamo tarehe 8 Juni 1960, Ganshof alisafiri kwenda Brussels kukutana na Mfalme Baudouin. Alitoa mapendekezo matatu ya mwezeshaji: Lumumba, mshindi wa uchaguzi; Joseph Kasa-Vubu, mtu pekee mwenye sifa ya kitaifa anayehusishwa na upinzani unaoungana; au mtu mwingine ambaye angeweza kuunganisha makundi yanayoshindana. Ganshof alirudi Kongo tarehe 12 Juni 1960.

**Itaendelea...**

# SAKO KWA BAKO:

## JULIANA ISONDO: MWALIMU MWENYE KIPAWA CHAKE

Na. Mwandishi wetu

Katika pitapita za Ngurumo ya Mwandishi mwezi huu *(Agosti 2022)* tumefika jijini Tanga. Huko kalamu yetu ikakutana na mwanadada mrembo, mwalimu wa shule ya upili anayeifanya kazi yake kwa moyo. Kwa muonekano wake na kujituma kwake, hakika anadhihirisha ule msemo wa 'Mwalimu Haiba'

Yafuatayo ni mahojiano mafupi kati yetu...

**1– Utambulisho wako kwa kifupi...**
Naitwa mwalimu Juliana Raymond Isondo, ni mama wa wengi na ni mwalimu kwa taaluma na mshauri kwa kipaji. Napatikana Tanga Bumbuli.
Ni mzaliwa kutoka Dodoma Tanzania. Msomaji mzuri wa vitabu.

**2- Nini kilikusukuma kuanzisha klabu ya usomaji vitabu?**
Kama mshauri wa wanafunzi shuleni kwetu, nilikuwa napokea *case* tofauti tofauti kutoka kwa wanafunzi. Nilipochunguza niliona zinasababishwa na ufinyu/uhaba wa maarifa sahihi. Hivyo basi niliamua kuanzisha *club* ya usomaji ili wanafunzi wapate maarifa kupitia mikasa na taarifa watakazozipata vitabuni.



Mwalimu Juliana Isondo (mwenye suti) pamoja na wanafunzi wake wa Shule ya Sekondari Soni jijini Tanga.

**3– Ni Changamoto zipi unazopitia katika kuendesha hiyo klabu?**
Katika kila jambo zuri changamoto hazikwepeki,
1. Uhaba wa vitabu. Tunakosa vitabu vya kusoma na ukisema wasome vitabu vya darasani wanakosa morali ya kuendelea na usomaji.
2. Muda.
Ratiba ya shule inatubana sana. Kuna wakati tunakosa muda wa kukutana na kuendelea na mijadala na uchambuzi.
3. Hamasa. Wanafunzi wengi wamekosa hamasa ya kuendelea na wengine kujiondoa kwenye usomaji wa vitabu.

**4– Je; kuna faida unazopata kupitia hiyo klabu?**
Wanafunzi wakipata maarifa yakawanufaisha, mimi nami nakuwa nimenufaika sana. Tunaishi kwa ajili ya wengine.

**5- Unawaambia nini waalimu wenzio kote nchini juu ya klabu kama hizi?**
Clubs za usomaji zinasaidia sana. Wazazi wengi wa kitanzania wanakosa muda wa kuzungumza na watoto wao.
Kupitia usomaji wa vitabu wanapata kufahamu mambo adhimu ambayo hata mzazi asingeweza kumfundisha/kumwelekeza mtoto wake.

**6- Nini malengo yako juu ya hiyo klabu yako**
Lengo kubwa ni kujenga mwamko wa kusoma vitabu bila kushinikizwa.

**7– Unawaambia nini wanaosoma andiko hili?**
Maarifa sahihi ni muhimu sana kwa kizazi chetu. Tupende kusoma vitabu na tupate maarifa kupitia majarida, makala na magazeti kama haya.

Mwl. Juliana Isondo ni mmoja waalimu wanaoandika sana maarifa mbalimbali kwa wanafunzi na wazazi kupitia jukaa la kijamii la Facebook. Ukitaka kujifunza kupitia kwake, ingia facebook mtafute kwa jina lake.

Katika toleo lijalo tutamleta tena ili tumjue zaidi.

# SHAJARA YA MUUAJI—9

Na. Richard Mwambe



**Jackson Balinga alipakiwa kwenye kalandinga na kupelekwa Keko kuanza kutumikia adhabu yake. Damu ya mtu haiendi bure!**

***Endelea..***

Aliwaza Amina aliyekuwa nyumba ndogo wa Sume Msamange. Aliapa na aliapa kuwa muuaji apatikane. Na aliahidi kwa afisa upelelezi Afande Steven kuwa atampa zawadi nono endapo atafanikisha muuaji kukamatwa. Kwa muungwana ahadi ni deni.

Mahakamani hapo pia alikuwapo mke wa Sume Msamange. Naye alikuja kuhakikisha muuaji anapatiwa adhabu. Uluka bado alikuwa anampenda mumewe. Kifo cha mumewe kiliukata katikati utamu alikuwa akiupata. Si kwamba alikuwa hajui kama kuna anayeshea naye, alijua vyema. Lakini hakuumiza kichwa, alifanya mahali pake.

Mara baada ya Mahakama kumalizika, kalandinga lile limeshaondoka, ndipo hatua za miguu yake zikamfikisha kwa Amina aliyekuwa mmoja wa mashuhuda. Uluka akasimama mbele yake tu, ana kwa ana, wakatazamana.

"Wote tumekosa, sivyo?" Uluka akamuuliza Amina. Amina akabaki kimya, hakujibu lolote, alijua nini maana ya swali lile. "Ulinichukulia kila kitu Amina... Hata chanzo cha mauaji kimetoka kwako... Mpenziwo Balinga ndiye aliyeua mume wangu... Asante, nawe ukipata wako nitakuja kumchukua," Uluka aliongea kwa uchungu. Akaondoka na kuingia kwenye gari. Wakatokomea!

Amina akabaki palepale aliposimama, mwili wake ulikuwa kama mtu aliyepigwa shoku ya umeme. Kwani uongo? Ndivyo ilivyo. Lakini kilichomuuma tu ni kuambiwa kuwa aliyeua ni bwana wake. Amina alimpenda Sume labda zaidi ya Uluka ambaye alikuwa mke wa ndoa. Si unajua mwanamke aliyeolewa husahau wajibu wake wa msingi nyumbani. Hii huwafanya akinababa kutafuta faraja upande wa pili. Ndivyo ilivyokuwa? Sijui. Siku ikapita, Jackson Balinga akawekwa jela... Ilikuwaje Hata akamuua Sume? Utata.

WP Ngai Matola, aliweka yale makabrasha vizuri mara baada ya kuyapitia harakaharaka na kuandika vitu vichache kwenye kijitabu chake. Katika uharaka huo wa kuperuzi yale majalada aliona pengo katika swala zima la kiuchunguzi la kesi ya mauaji ya Aziza na Sume Msamange.

Lilishapita, lakini Ngai alijkuta akitaka kurudisha siku nyuma. Si kwa ajili ya mtu yeyote bali kwa kujiburudisha tu. Alipenda kuburudika kwa mtindo huo. Sijajua kwanini lakini alipenda. Tangu akiwa mwanafunzi alipenda sana kusoma vitabu vya kipelelezi, alipenda kusoma makala za kichunguzi na hapo angemkaba baba yake kwa maswali yasiyo na ukomo. Alipokuwa shuleni alipenda kutetea walionyimwa haki na kuwaweka hadharani wale wote wenye makosa kihalali.

WP Ngai Mathola alijikuta na furaha sana kila auanikapo ukweli. Hii ilimkosanisha na kaka na Dada zake mara nyingi kwa kuwa ye' ndiye aliyekuwa msema kweli hapo nyumbani kwao. Sasa amekuwa mkubwa. Amejiunga na jeshi la polisi. Yote hayo yalikuwa ni Neema na baraka za marehemu baba yake. *'Unafaa kuwa polisi tena mpelelezi'*.

Kauli hii haikumtoka kichwani. Mara baada ya kuhitimu masomo yake ya kidato cha sita alijiunga na jeshi la polisi kisha akajiendeleza kielimu. Sasa alikuwa na nyota moja begani. Siku hii Ngai alijikuta mwenye furaha sana. Alikwishapanga mkakati wake wa kuifanya ile kazi kama sehemu yake ya burudani. Alijipanga kuutumia muda wake wa ziada kufuatilia jambo moja moja katika hizo kesi ikiwemo wahusika ambao walikwishawahi kuhojiwa na polisi lakini wapo nje.

Kwenye rafu mojawapo, pembeni alikuwa bado ana majalada matatu mengine ya mauaji ambayo bado alikuwa hajayapitia kuona kilichomo. Ila katika haya ya awali,

mawili yalishamfanya atamani kuyafanyia kazi hasa kwenye mapungufu aliyoyaona. Alihitaji kufika Mibingiriko Gesti Hausi, alihitaji kuonana na Amina lakini zaidi ya yote alitaka kukutana na hata walioendesha hiyo kesi huko mahakamani. Ijapokuwa aliogopa kwa kuwa ni kosa kufanya kazi bila maagizo ya mkubwa wako, Ngai alipiga moyo konde. Ujeuri nao wakati mwingine una chanya zaidi ya hasi.

Akakusanya yale majalada mengine yaliyobaki na kuketi kitako. Akaanza kupekua moja baada ya jingine. La kwanza lilikuwa la mwanamke aliyemkata dhakari mume wake, kisa ni wivu wa mapenzi. *Dunia ina mambo! Kuwakosesha raha tu wengine.*

Ngai akasoma maelezo yale kwa tuo. Akaelewa. Mapenzi yanauma, hasa umpendaye akikusaliti. Akatikisa kichwa, hakumlaumu mwanamke huyo kwa alilofanya. Alijua ni hasira. Usiamue jambo ukiwa na hasira maana wazee walisema 'hasira hasara'. Akaliweka kando.

Akachukua lingine, hilo nalo lilikuwa na maelezo ya mama kuua mwanae wa mwaka mmoja kwa kumpa sumu, kisa eti baba haleti matumizi. Walishaachana. Ngai alisikitika kwa uhai wa mtoto kukatishwa. Mtoto hakuwa na kosa kwanini umkatishe uhai wake? Changamoto za kifamilia. Akaliondoa na kuliweka kando.

Kabrasha la tatu, hili ndilo liliitikisa akili yake. Ngai Mathola, WP mwenye nyota moja begani pake, alijikuta akiingiwa na ubaridi ulioanzia utosini mpaka unyayoni. Lilikuwa jarida la mauji. Mauaji hayakuwa ya raia bali askari polisi mwenye cheo kikubwa tu cha ASP. Mauaji hayo yalifanyika hapo Sugar Ray, kona maarufu ya machangudoa katika Wilaya ya Temeke. Ngai akapekuwa karatasi kadhaa, akakutana na maelezo ya mwanadada mmoja na mmiliki wa baa hiyo. Taarifa ya uchunguzi wa kipolisi ilionesha marehemu aliuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali. Maelezo ya aina ya jeraha yalishahabiana na Yale ya kifo cha Aziza na Sume. *Kuna nini hapa?* Akajiuliza. Ngai akameza mate. Kama ni muvi ndiyo hii hapa!

**Tsh 4000/= Softcopy. Lipia Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Whatsapp 0766974865**

*Haya majalada matatu yana mauaji ambayo yanataka kufanana kwa namna fulani!* Akawaza. Ilikuwa ni rahisi kujua kwanini pamefanyika kosa kama hilo. Marehemu waliuawa siku tofauti, miezi tofauti japo miaka michache tu iliyofuatana. Wapelelezi waliofanyia upelelezi kesi hizo walikuwa watatu tofauti. Hivyo isingekuwa rahisi kuoanisha hizo tafutishi ili kujua kuwa muuaji ni mmoja. *Hata ingekuwa mimi, ningefanya hivihivi!* Akawaza.

Jalada hili la mauaji ya ASP Mjigwa nalo lilikuwa limefungwa ina maana lazima kuna mtuhumiwa keshakuwa mfungwa wa mauaji haya. *Wako sahihi!* Ngai akafunga lile jalada baada ya kunukuu vitu vichahe alivyovihitaji kwenye kile kijitabu chake. Akainuka na kuelekea kaunta. Pale alikuta askari wengine kama watano hivi wakishughulika na wateja waliofika hapo kuwasilisha shida zao mbalimbali. Akamgusa begani yule ambaye kidogo alikuwa na unafuu na kazi. Yule kijana akasimama kwa ukakamavu na kutoa saluti, maana Ngai alikua juu kwa cheo.

"Samahani afande, swali dogo... Najua we umekaa hapa Chang'ombe miaka mingi kidogo..." Akamwambia.

"Ndiyo afande!" Akajibu yule PC

"Unamfahamu Inspekta Damasi na Steven ?"

***Itaendelea toleo lijalo***

**“Show time!” akajisemea huku akiingia Barabara ya Old Bagamoyo na kuelekea Kawe. Baada ya kupita kidogo Mikocheni B akateremka kulia kwa upande wa Msasani na kufika katika club hiyo.**

***Endelea..***

Nje kulikuwa na magari mengi ya kifahari maegeshoni, naye akaegesha la kwake na kubaki ndani akisubiri kuona katika dakika tano nini kitatokea.

Hazikufika hata hizo dakika tano Toyota Harrier moja likaingia kwa fujo eneo lile na kuegeshwa. Kijana mmoja mwenye siha ya kimazoezi haswa, alishuka na kuubamiza mlango nyuma yake. Wakati huo huo Amata akachukua simu yake na kuipiga tena akimtazama kama atainua mkono kuipokea au la. Na hilo ndilo lililotokea.

*Mjinga sana, umenasa mwenyewe sasa utanijua mi nani!* akajisemea na kushuka garini, kisha akaenda kulekule ndani ya klabu hiyo.

Alipoukaribia mlango mkubwa tayari akaanza kusikia mzozo. *Kumekucha!* Akawaza huku akiingia taratibu na kumkuta Carlos akiwa ameshikwa na watu watatu wenye miili mikubwa. Akachukua simu ya Marietha na kuipiga ile ya yule mwanamke aliyempigia kwanza, lo, kumbe hakukosea. Simu moja iliyokuwa mezani ikawakawaka, na jirani hapo kulikuwa na mwanamke anayelia kwa uchungu. Amata akateremka taratibu mpaka katika ile meza, akatoa kitambulisho.


“Polisi Ofisa, kaa chini!” akamwamuru Carlos, lakini hakutii, “kaa chini kabla sijatumia nguvu kukuweka hapo,” akaongeza kusema. Wale vijana waliokuwa wamemshika na walionekana ndiyo mabaunsa wa ukumbi huo walimwachia.

“Tii sheria bila shuruti, nimekwambia kaa chini hutaki kusikia unataka dola itumie nguvu sio?” Amata akaunguruma lakini Carlos bado alikuwa kasimama akionesha uanaume wake. Hakumpa hata sekunde kumi, alimkamata na kumchota mtama mmoja maridadi, Carlos akaenda chini kama mzigo kisha akamkanyaga kifuani kwa nguvu.

“Jamani mme wangu mtamwua!” yule mwanamke akapaaza sauti akiinuka kwenye kile kiti na kwenda pale alipo Amata.

“Tulia!” akamwambia yule mwanamke, “ungekuwa unampenda usingemsaliti?” wakati anaongea hayo, Carlos kutoka pale chini akaukamata mguu wa Amata na kuunyonga kwa nguvu. Kamanda aliliona hilo akajizungusha na mguu mmoja ukahamia upande wa pili. Akajitoa kwenye himaya ya kijana huyo. Kutoka pale chini akajibetua na kusimama wima. Akarusha ngumi kwa Amata ikaepwa, ya pili ikaepwa, ya tatu, ikadakwa. Amata akamvuta kwake kwa nguvu na kumpiga kichwa kilichotua barabara kwenye mwamba wa pua, kisha akamsukuma kando. Kwa mruko mmoja hewani akajizungusha na mateke yote mawili yakamwishia Carlos. Carlos akatua juu ya kiti na kukitawanya vipande viwili. Kwa haraka akainuka na kujipanga kwa mapigano, alipopeleka pigo hilo kwa minajiri ya kumaliza kazi, Amata alilipangua vyema na kumpa pigo moja la karate lililotua mbavuni, pigo la pili likapiga eneo la chembe kisha akapiga ngumi katikati ya kolomeo, Carlos akapiga magoti.

Kamanda Amata akachomoa pingu kutoka katika suruali yake, “mvalisheni” aka-




waambia wale mabaunsa nao wakafanya kazi hiyo kisha akamkokota na kutoka naye nje. Alipofika tu nje ya club hiyo alikuta gari la polisi ‘nyuki’. Wale vijana wa polisi wakateremka na kumnyanyua wakamtupia ndani ya Defender, na Amata akadandia nyuma yake.

“Twendeni kituoni moja kwa moja!” akawaamuru baada ya kuwaonesha kitambulisho chake cha upolisi feki, wakaondoka kuelekea Oysterbay.

❦

Carlos alitupwa kwenye chumba tupu, ndani yake alikuwa peke yake, hakukuwa na mtu mwingine. Amata alitulia nje, na mara kwa mara aliingalia saa yake.

“Afande vipi kuhusu huyu mtu wako?” mmoja wa askari aliyekuwa akikaimu nafasi ya mkuu wa kituo alimuuliza.

“Kuna watu nawasubiri, watafika muda si mrefu,” alipojibu hilo tu akaona BMW jeusi likikunja kushoto kisha kulia kuingia eneo hilo, “yes!” akasema huku akiteremka chini kutoka pale juu ali-

pokuwa amesimama. Madam S aliwasili kituoni hapo, akateremka na kukutana na Amata.

"Una uhakika mlengwa ndiye?" akamuuliza.

"Mi sio mgeni wa kumkamata mtuhumiwa…"

"Ok!"

Wakati wakiongea hayo, Toyota Altezza jekundu nalo likakunja kona kuingia katika wigo huo wa kituo cha polisi Oysterbay. Chiba aliwasili. Akateremka na kimkoba chake kidogo kisha akaungana na wenzake wote wakaingia ndani ya kituo hicho.

"Afande mbona sikuelewi? Hawa ni akina nani tena?" akauliza yule askari mwenye vyeo vichache begani mwake. Wakatoa vitambulisho halisi, wote watatu, na yule afande akagwaya. Baada ya kugundua kuwa serikali ilikuwa hapo. Wote watatu wakaingia ndani ya chumba kile wakamkuta Carlos akiwa pembeni kaegemea ukuta kimya.

"Carlos Zejack De Santos!" Amata akaita wakati Chiba tayari ameshatega chombo chake cha kunasa mazungumzo. Aliposikia jina lake akatazamana na Amata moja kwa moja, kisha akwatazama wale wengine waliokuwa kando.

"Naomba ndoo yenye maji na kitambaa kizito!" akamwomba yule askari naye akatuma vijana na vyote vikafanyika, "muinueni na pingu zake muwekeni kwenye kiti hiki," wale vijana wa polisi wakafanya hivyo.

"Carlos, yuko wapi Marietha? Msichana anayefanya kazi Mapokezi katika hoteli ya Vatican Wing?" akauliza.

"Simjui… sasa sijui nitakujibu nini!" Carlos akajibu kijeuri.

"Ujeuri wako hautakusaidia kabisa, toa ushirikiano. Najua wazi kuwa wewe ndiye uliyemteka Marietha leo jioni nyumbani kwake Kimara ukishirikiana na mwanamke mmoja kibonge. Mimi nilikuwa nyuma yenu kwani nilijua nini mnataka kufanya. Yuko wapi Marietha? Sasa sicheki!" akamwuliza kisha yeye akasimama. Carlos akabaki kimya, hakujibu lolote.

"Dawa ya moto ni moto!" akasema Amata na kukibetua kile kiti kama anakiangusha kwa nyuma wale vijana wakakidaka na kikawa kimeinama kikimwacha Carlos akiangali juu, akachukua kile kitambaa na kumfunika usoni kisha akachukua yale maji na kummiminia usoni. Maji yalimwingia puani, na kumsumbua, Carlos akajikuta anataabika na kushindwa afanyeje, akapiga makelele kwa shida, wakamwinua.

Akakohoa na kutema maji mengi. Kila alipohema, pumzi yake ilitoka na maji, "mtaniua ninyi, mtaniua! Khoh khoh khoh"

"Na lazima ufe kama usiponipa majibu ya maswali yangu," Amata akamwambia kisha adhabu ileile ikarudiwa tena kwa dakika moja zaidi.

"Aaah, ops! Gulp, gulp…. Khooooo!" Carlos akaanza kukoroma, wakamwinua, akatapika maji mengi na kupiga chafya kadhaa.

"Yupo Kawe, Kawe!" akajibu.

"Kawe kwa nani?"

"Mafichoni, mafichoni…"

"Ok, good," Amata akajibu, "kwa nini mmemteka?"

"Mariet-tha ana m-zi-go wetu" akajibu kwa kusitasita huku akipiga chafya mfululizo. Kidogo simu ya Carlos ambayo ilikuwa pembeni ikaanza kuita, Amata akainyanyua akaiangalia ile namba, Hellen!

"Hellen ndio nani?"

Kwa swali hilo, Carlos akatulia na kutoa macho.

"Jibu Hellen ndiyo nani?"

"Yup-po Ka-we!" akajibu.

"Sawa," Amata akatulia na ile simu na kuanza kupekuwa jumbe mbalimbali zilizoingia katika simu hiyo na kuzikuta za kutosha, na kumbana kumuuliza maswali mengi sana ambayo aligoma kuyajibu. Amata akamtazama Madam S, kisha akamwuliza kwa macho.

"Mpeleke Shamba tukafahamiane vizuri," Madam akasema  na wakati huohuo mlango ukagongwa. Ulipofunguliwa, Scoba aliwasili na Dkt. Jasmin.

"Mleteni huku," akawaamuru wale polisi nao wakafanya hivyo, kabla hajashushwa ngazi za nje, akavalishwa guo jeusi usoni, na kushushwa kisha akatupiwa kwenye Land Cruiser aliyokuja nayo Scoba. Pamoja naye, Chiba na Madam S wakafuatana na gari hilo wakimuacha Amata na Dkt Jasmine.

"Mkuu, naomba vijana na gari kuna mtu tunaenda kumchukua," Amata akamwomba yule askari aliyekuwa akikaimu nafasi ya ukuu wa kituo muda ule. Haikuwa shida, akaruhusu lile gari la vijana wa kazi kufuatana na Amata kwenda Kawe. Usiku huohuo Amata aliwasili na askari wale mbele ya jumba hilo ambalo kwalo Marietha alihifadhiwa.

***Itaendelea toleo lijalo..,.***

**"nitamuomba kaka yangu anisaidie," mtengeneza mitungi alijisemea moyoni. " na shemeji yangu pia atanisaidia. Kama tukifanya kazi hii kwa juhudi, natumaini tutaimaliza ndani ya huu muda wa wiki moja."**

Baada ya wiki moja mitungi ile ilikuwa tayari, kiongozi wa wezi akaenda kwa muuza mafuta mkubwa sokoni na kujaza mtungi mmoja mafuta. Kisha akamtuma mmoja wa wezi akawalete wale punda ishirini aliowanunua.

Kiongozi wa wezi akapakia kwa kila punda mitungi miwili miwili. Kisha akawapeleka mpaka kule msituni kukutana na wezi wengine waliobakia huko.

"Sasa ni sehemu ya pili ya mpango wangu," alisema kiongozi wa wezi. "Kila mmoja wenu aingie ndani ya mtungi mmoja."

"Tuingie kwenye mitungi? Kwanini?" aliuliza mmoja wa wezi . "Na tutapumuaje?"

"mifuniko yake haikazi sana." Alijibu kiongozi wa wezi. "Msihofu – mtaweza kupumua. Chukueni panga zenu na ngao muingie nazo ndani ya mitungi kwasababu zina kazi yake maalumu huko. Tutaenda kwenye ile nyumba mkiwa nyote thelathini na tisa ndani ya mitungi thelathini na tisa."

"Na vipi kuhusu huo mtungi wa arobaini? Utaingia wewe?" mmoja aliuliza.

"Hapana!" alijibu kiongozi wao. "Nitavaa mavazi ya kuficha uso na nitawaongoza punda wote mpaka huko. Huu mtungi wa arobaini umejaa mafuta – ni moja ya mpango wangu, nitajifanya ni muuza mafuta. Nitawaongoza punda wote mpaka kwenye nyumba ambayo Mustafa alinionesha. Nitawaomba watu wa nyumba ile kama watanipa msaada wa kulala usiku mmoja kwasababu niko kwenye safari ndefu na ninapoelekea ni mbali sana. Kisha akiniruhusu tu na kunipa nafasi ya kuwaingiza punda hawa ndani, sasa itakuwa ni nafasi yenu nzuri ya kujitokeza na kumaliza kazi. Hapo atajuta kutuibia mali zetu."

Baada ya kusema hayo kila mwizi alichukua upanga na kuingia ndani ya ile mitungi.

Kiongozi akavaa mavazi ambayo uso wake hauwezi kuonekana vizuri, kisha akaanza safari ya kuelekea mjini na punda ishirini waliobeba mitungi arobaini.

Muda ambao alikuwa ameshafika mjini, tayari giza lilikua limeshaanza kutanda. Muda mfupi tu akafika katika nyumba ile yenye maua mazuri na paka wa rangi ya machungwa. Kulikuwa na mtu aliyekaa kwenye stuli nje ya nyumba hiyo. Alikuwa akitazama watu wanaopita njia na akisikiliza sauti za ndege mbalimbali wakiwa wanatoa sauti za kujibembeleza kwaajili ya kulala.

Kiongozi wa wezi alipomuona yule mtu nje, alisimamisha punda wake wote.

"Habari ya saa hizi." Kiongozi alimsalimia Alibaba.

"Nzuri," alijibu Alibaba kwa hali ya kushangaa na kusimama kwa kuheshimu mgeni. "Naitwa Alibaba. Naweza kukusaidia nini rafiki yangu?"

"Mimi ni muuza mafuta, natokea mbali sana." Alijibu yule kiongozi wa wezi. "Punda wangu wamechoka sana na hata mimi vilevile. Tunaweza kukaa kwako usiku huu tu kisha kesho asubuhi tutaondoka. Hatutakuwa na usumbufu wowote tafadhali."

"Umesema wewe ni muuza mafuta. Mafuta hayo yako wapi?" aliuliza Alibaba kutaka kuhakikisha kwamba yule mtu ni mkweli."

Yule kiongozi wa wezi akamuoneshea kwenye ule mtungi ambao alijaza mafuta. "Yapo kwenye mitungi hii, ni mafuta bora na mazuri sana kuliko ya aina yoyote ile. Ungependa kuyaona?"

Akafungua mfuniko wa ule mtungi wenye mafuta na Alibaba akachungulia ndani yake. Kisha akanyanyua macho kumtazama kiongozi na kutabasamu.

"Karibu sana ndani ukae," alisema Alibaba. " Walete punda wako



# TET YAZINDUA NA KUGAWA VITABU VYA USHINDI

TAASISI ya Elimu Tanzania, chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imefanya uzinduzi wa ugawaji wa vitabu vilivyoshinda Tuzo ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu kwa mwaka 2022/2023 na kimoja cha 2023/2024.

Katika hafla hiyo iliyofanyika mwezi Novemba tarehe 19 katika viwanja vya taasisi hiyo, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia alisema, "Tuzo hii itaendelea kuchochea waandishi wengi kuandika vitabu vizuri na vyenye maadili ambavyo vitasaidia katika kutumika shuleni kwa watoto wetu. Na hii itasaidia sana Watanzania wengi kupenda kujisomea vitabu vilivyoandikwa kwa lugha yao ya Kiswahili."

Pia ameeleza kuwa serikali itaendelea kuipa nguvu Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) katika kuhakikisha tuzo hii inaendelea kila mwaka na kushirikisha watu wengi na kufanya soko la uchapishaji wa vitabu vya hapa nchini lizidi kukua. Vilevile, serikali itaendelea kuhakikisha waandishi wote nchini wenye vipaji wanafikiwa na kushiriki na kuwasilisha miswada yao kwa ajili ya tuzo ya mwaka 2024/2025 kwa wingi.

Aidha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo imeipongeza TET kwa uratibu wa Tuzo ya Taifa ya Uandishi Bunifu ya Mwalimu Nyerere na kukamilika kwa uandishi vitabu vya mitaala iliyoboreshwa.

Naye Mkurugenzi wa TET, Dkt. Aneth Komba, ameeleza kwamba vitabu vyote violivyoandaliwa kwa kupitia maandiko ya washindi hao wa tuzo vitaanza kusambazwa shuleni ili wanafunzi waweze kujifunza.

Vitabu hivyo ni Zawadi (Hadithi za watoto), Gereza la Kifo (Riwaya) na Mtale wa Ngariba (Ushairi) vimechapishwa kwa udhamini wa Serikali na Benki ya Dunia.

Katika hafla hiyo pia imesisitizwa kwa Watanzania kujitokeza kuwasilisha miswada yao kwa ajili ya kushindaniwa.



Shafi Adam Shafi akiwa na washiriki wengine kwenye hafla ya uzinduzi na ugawaji vitabu vilivyoshinda Tuzo Nyerere 23/24




**Waziri wa Elimu Prof. Adolf Mkenda katika picha ya pamoja na baadhi ya wageni waliohudhuria hafla ya uzinduzi na ugawaji wa vitabu vilivyoshinda Tuzo Nyerere 23/24**

## Unajua nini kuhusu historia ya rafu za vitabu na maajabu yake?

**Ni nani aliyegundua rafu (Shelf) ya vitabu ulimwenguni?**

Hakuna mtu mmoja aliyegundua au kubuni wazo la "shelf ya vitabu" duniani kwa sababu ni wazo la asili ambalo linaweza kufuatiliwa nyuma katika historia ya binadamu tangu enzi za zamani.

Wakati wa ustaarabu wa kale, kama vile Wamisri wa kale, Wagiriki, na Warumi, walikuwa na njia za kuhifadhi maandishi na maandiko. Hifadhi ya vitabu, kama maktaba ya Alexandria iliyojengwa karibu na karne ya 3 KK, ilihusisha aina fulani ya *shelving* kwa ajili ya vitabu vya kifungu.

Katika historia ya hivi karibuni, *shelves* za vitabu (kama tunavyojua leo) zilianza kuboreshwa zaidi wakati wa karne ya 16 hadi 18, wakati wa enzi ya Mwangaza, ambapo vitabu vilianza kuchapishwa kwa wingi na matumizi ya maktaba binafsi yaliongezeka. Katika muktadha huu, shelves za vitabu zikawa kipengele cha kawaida nyumbani na kwenye taasisi za elimu.

Kwa hivyo, shelf ya vitabu ni uvumbuzi wa pamoja wa ustaarabu mbalimbali, uliokuja hatua kwa hatua kutokana na mahitaji ya kuhifadhi na kupanga maarifa yaliyoandikwa.

**Je ni rafu (shelf) gani kubwa kuliko zote?**

Rafu kubwa zaidi ya vitabu ulimwenguni iko Kansas City, Missouri, Marekani. Ni sehemu ya *Kansas City Public Library* na inaonekana kwenye ukuta wa jengo la maegesho ya magari. Muundo huu wa kuvutia unaonyesha "rafu ya vitabu" yenye mgongo wa vitabu vikubwa 22, kila kimoja kikiwa na urefu wa futi 25, ikiwakilisha tamasha la kuona la fasihi ambalo linachukua kitalu kizima cha jiji. Majina ya vitabu kwenye mgongo huo yalichaguliwa kwa maoni ya jamii na yanawakilisha mchanganyiko wa kazi za jadi na maarufu.


Kwa upande wa maktaba yenye mkusanyiko mkubwa zaidi duniani, hiyo ni *Library of Congress* huko Washington, D.C., yenye zaidi ya vitu milioni 170, ikiwa ni pamoja na vitabu, maandiko, na rasilimali za *multimedia*.

Je rafu hiyo ipo katika rekodi za dunia za Guiness?

Shelf kubwa ya vitabu katika *Kansas City Public Library,* inayojulikana kama *Community Bookshelf*, haijaorodheshwa rasmi katika Kitabu cha Rekodi za Dunia cha *Guinness* kama rafu kubwa zaidi ya vitabu. Ingawa inajulikana sana kwa ubunifu wake wa kipekee wa usanifu—ukuta wa maegesho uliobadilishwa kuonyesha safu ya vitabu vikubwa—hakuna ushahidi kwamba imepewa tuzo yoyote rasmi na *Guinness*.

Hata hivyo, muundo huu umepata umaarufu mkubwa ulimwenguni na kuvutia wageni kwa ubunifu wake wa kisanii na wa kuvutia. Ni alama mashuhuri ya Kansas City na chanzo cha fahari kwa jamii ya eneo hilo.

Hapa kuna picha ya rafu kubwa ya vitabu katika Kansas City Public Library, inayojulikana kama *"Community Bookshelf."* Ubunifu wake wa kipekee huonyesha safu ya vitabu vikubwa, na ni kivutio kikuu cha usanifu. □




Imeandaliwa kwa msaada wa mtandao

# KITABU NILICHOSOMA

KITABU: **The Richest Man in Babylon**
MWANDISHI: **George S. Clason**
MSOMAJI: **Godlisten Given**

Mafunzo makuu niliyopata kwenye kitabu cha The Richest Man in Babylonn kama ifuatavyo:

1. KUJILIPA KWANZA *(PAY YOURSELF FIRST)*
Kitabu hiki kinafundisha umuhimu wa kuweka akiba kwanza kabla ya kutumia fedha zako.
- Kila kipato unachopata hakikisha unaweka angalau 10% kama akiba.
- Hii itakujengea nidhamu ya kifedha na huandaa kwa siku za mbeleni.

2. ISHI CHINI YA KIPATO CHAKO (*LIVE BELOW YOUR MEANS)*
Mwandishi anashauri kutumia kiasi kidogo kuliko unachopata kutoka kwenye vyanzo vyako vya mapato.
- Epuka matumizi yasiyo ya lazima na madeni chefuchefu.
- Matumizi yenye tija yatakuongezea akiba na kutengenezea mazingira mazuri ya uwekezaji.

3. FANYA PESA ZIFANYE KAZI KWAKO (*MAKE YOUR MONEY WORK FOR YOU)*
Mwandishi Clason anasisitiza umuhimu wa kuwekeza akiba yako kwa faida.
- Wekeza katika fursa zinazoaminika ili uzalishe kipato cha ziada.
- "Fedha zinapaswa kuzalisha fedha zaidi," yaani, uwekezaji unapaswa kurudisha faida.

4. TAFUTA USHAURI KUTOKA KWA WATAALAMU. (*SEEK ADVICE FROM EXPERTS)*
Moja ya funzo kubwa ni kutafuta ushauri kutoka kwa watu wenye maarifa sahihi.
- Usifanye maamuzi ya fedha ukiwa na ujuzi mdogo juu ya jambo lolote.
- Sikiliza waliofanikiwa kabla ya kuwekeza au kutumia pesa zako usije ukajuta bure.

5. UVUMULIVU NA KAZI KWA BIDII *(PERSEVERANCE AND HARD WORK)*
Mafanikio hayawezi kupatikana mara moja, inahitaji mtu mwenye sifa ya uvumilivu.
- Juhudi za mara kwa mara na nidhamu ni muhimu katika safari za mafanikio.
- Changamoto za muda mfupi zinaweza kuwa sehemu ya safari ya mafanikio ya muda mrefu.

Kwa ujumla, kitabu cha *The Richest Man in Babylon* kinatoa mafunzo ya kimsingi kuhusu usimamizi wa fedha, kikilenga kukusaidia kukuza nidhamu ya kifedha kwa wewe na mimi ambaye tunatamani kuwa na utajiri wa kudumu.

Namshukuru mbeba maono wa *Anna Mbise Mobile Library* kwa kutochoka kunihimiza kupata maarifa kupitia vitabu nakiri kujengwa na kuimarika kila siku.

Wanafamilia wote tusome vitabu.

***Wole Soyinka… inatoka ukurasa wa 8 na 9***

Ndoa yake ya pili ilikuwa 1963 na mfanyakazi wa maktaba wa Nigeria, Olaide Idowu, ambaye alizaa naye binti watatu - Moremi, Iyetade (1965-2013), Peyibomi - na mwana wa pili, Ilemakin. Binti mdogo wa Soyinka ni Amani. Soyinka alifunga ndoa na Folake Doherty mwaka wa 1989 na wanandoa hao wana watoto watatu: Tunlewa, Bojode na Eniara.


Soyinga ametimiza miaka 90 mwaka 2024.

***Kutoka Facebook***

# HABARI PICHA




Hussein Issa Tuwa wa pili toka kulia na wadau wengine waliohudhuria katika uzinduzi wa kitabu cha MAISHA YANGU NA KAKA MWENYE USIONJI kilichoandikwa na Baraka Ibrahim (11)




MTALE WA NGARIBA moja ya vitabu viliyozinduliwa na TET.




Picha ya kupendeza… waandishi ambao vitabu vyao viliibuka nkidedea Tuzo Nyerere' 2023 na 2024 katika picha ya pamoja na wadau wa Kamati ya Tuzo hiyo.



**BIMA YA PENZI mpaka Uganda. Katika toleo lijalo tutakuletea makala maalum ya safari ya Goima huko Uganda kuipeleka Bima ya Penzi.**

CHRISTMASS hii ikawe ya heri kwako na familia yako. Mwenyezi Mungu akubarikini na awajaze amani.

Nyote muwe na mwaka mpya mwema wenye mafanikio tele, mfun-guliwe milango ya neema kiroho na kimwili.

*Richard Mwambe*

**TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.**
**Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.**
**Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

# MALENGA WA KILEO

## KARIAKOO

Kariakoo Kariakoo Kariakoo
Nakuita mara tatu,
Vimesikika vilio
Vya uchungu wa watu,
Una nini Kariakoo
Kuwatwaa ndugu zetu?

Mioyo yetu yalia
Chozi kububujika,
Ndugu twawalilia
Huzuni imetubaka
Una nini Kariakoo
Kutuliza namna hii?

Umezizima ndoto
Za vijana damu changa,
Wamekufa kwa joto
Na kifusi cha mchanga,
Una nini Kariakoo
Mbona twashindwa jipanga?

Ni habari ilo mbaya
Asubuhi yatufika,
Wamekufa si kwa ubaya
Maafa yaliwafika
Una nini Kariakoo
Kipi kilichofichika?

Maulana wapokee
Waja walotangulia,
Tena uwape afue
Wahanga walobakia,
Una nini Kariakoo
Mbona tunakuogopa?

Poleni mlofiliwa
Nanyi mlojeruhiwa,
Sisi sote tumefikwa
Na janga zito la ukiwa
Una nini Kariakoo
Macho twakukodolea

***Amani Msuya***
***Arusha***

## NIMUOE AMA NIMWACHE?

Nini niseme usikie?
Kilio gani wataka nilie?
Najua kuwa ni bintie
Nimuoe ama nimwache?

Kwanza hajui jiko
Wala kukalanga diko
Kutwa kucha ni mitoko
Nimuoe ama nimwache?

Kwa sura kasurika
Kwa umbo kaumbika
Tabiaye nataabika
Nimuoe ama nnimwache?

Hajui kutulivika
Ampendaye kumshika
Kitandani patashika
Nimuoe ama nimwache?

Ndoa ajitahidi ishi
Harusi hajui ishi
Hataki pokea michi
Nimuoe ama nimwacha?

Mtaani wanasema
Kaonjwa na kila mwema
Ndani mkaidi nje mama huruma
Nimuoe ama nimwache?

Kama humjui hutomjua
Jukwaale alijua
Shere atakuzuzua
Nimuoe ama nimwache?

Nimuoe ama nimwache, ndilo nalokuuliza
Kwani haya ni machache, juu yake kukujuza
Ndani atemapo cheche, mimi huyo hutereza
Nimuoe ama nimwache?

***Bakari Jamari***
***Mdau wa Ngurumo,***
***Mang'ula.***

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
"Siku zote usipuuze vitu unavyoviona vidogo... maana vidogo ndivyo vyenye madhara makubwa"
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
Jikamatie
Nakala Yako
DAR ES SALAAM
Duka la Kona ya Riwaya
Kinondoni Morocco
Simu:
0655428085
Zammira

# KUTOKA MAKTABA: MAISHA NI MAPAMBANO—5

**Hiki ni kitabu kilichoandikwa miaka mingi sana nyuma. Kiliandikwa ili kiweze kusomwa na watu mbalimbali na kuwekwa kwenye maktaba za vijijini. Tunakitoa kutoka kwenye maktaba yetu ili kukupa uhondo, Ngurumo ya Mwandishi ni kisima cha fasihi chenye hazina iliyotukuka.**

## TAMAA YA UTAJIRI WA HARAKA HARAKA—5

Mpepo na Luzolo waliytafakari mawaidha ya wasafiri hao. Lakini walikuwa na imani kuwa wasingepatwa na mikasa kama hiyo badala yake bahati ilikuwa yao.

Siku ya pili usiku, waliingia katika eneo la Tunduma. Wakaulizia wenyeji, maana Luzolo alikuwa anafahamiana na baadhi ya vijana wa sehemu ile ambao ndiyo waliompasha habari na kumshawishi juu ya habari za uchimbaji madini. Kadhalika Luzolo kwa zamu yake akamshawishi Mpepo.

Walifanikiwa kupata watu wanaowafahamu. Wakashirikiana nao. Kwa vile walikuwa wamechoka kwa safari ya miguu, walipumzika kwa siku mbili na huku wakikusanya vifaa vya kufanyia kazi. Vyote vilipatikana kwa njia ya kuzima na kukodi. Hakika walitegemea mafaniko yangekuwepo.

Baada ya mapumziko, wenyeji walikwapeleka kwenye maeneo ambayo yalikuwa na dalili ya madini, kule Mkuze. Utaratibu wao ni kwamba hawachimbi karibu karibu. Wanapeana maeneo u,nali wa kiasi cha kilometa tano kutoka kila mtu au kikosi. Eneo ambalo mtu au kikundi kinaruhusiwa kumiliki ni eneo lenye mzunguko wa kilomita tano. Hiyo inakuwa himaya yake au ya kikundi. Mtu mwingine haruhusiwi kuingilia. Hii ni sheria ya huko porini.

Mpepo na mwenzake walianza kazi. Kazi haikuwa rahisi maana walipata shida. Ili kutoharibu utamu wa mkasa wenyewe, yafuatayo ni masimulizi ya Mpepo mwenyewe:

“Nikueleze nini? Tulianza kuchimba na kuvunja miamba haraka haraka. Siku tano zilipita, kila siku tukichimba kwa bidii mchana kutwa. Hatukuweza kuifanya kazi ile usiku kwa hofu ya wanyama ambao walikuwa wakitawala eneo lile. Tulichimba na kuchekecha mchanga kwenye karai biala kuona dalili ya madini kwa muda wa siku zote tano. Luzolo alikumbuka nyumbani, akawa anaongea mambo ya ajabu. Mara hatukutambika, mara uaminifu wa mkewe huko nyuma ulikuwa na mashaka, na mengine mengi yaliyoandamana na miiko.

Juhudi yetu kubwa iliambatana na ujinga. Maarifa yalituambaa katika kazi ile. Tukakata tamaa tukaamua kurudi mjini Tunduma ili kutembelea maeneo mengine tofauti ambayo yalikuwa na dalili ya madini. Miaka miwili ikapita bila mafanikio wala huruma kwetu. Tatizo la kuishiwa chakula na maji mara kwa mara, halikuwa geni kwetu. Wakati mwingine tulichimba shimo mbugani lililokuwa na kina cha hata meta kumi. Hakuna tulichopata ila maji safi na salama kitu ambacho kilikuwa hadimu sana sehemu zile. Miili yetu ilianza kudhoofika kwa kuandamwa na chawa na wadudu wengine.

Mpepo na rafiki yake waliendelea na juhudi zao ingawa sasa matumaini yalikuwa yanafifia. Tukio baya zaidi ni siku walipokamatwa na askari kwa sheria ya wizara ya madini. Hawakuwa na leseni, wala sehemu ile haikuwa imeruhusiwa kwa uchimbaji wa aina yoyote wa madini. Walipelekwa kituoni kujibi maswali kuhusiana na wizi wa mali ya asili ya umma.

Kule nyumbani kwao Mpepo ma Luzolo kulikuwa na wasiwasi mkubwa. Habari za mchanganyiko zilikuwa zinatolewa mara kwa mara na wastu wasiohusika. Wengine walikuwa wanasema Mpepo na Luzolo waliliwa na tembo, wengine samba. Pia watu wengine walijigamba kuwa waliwaona kwa macho yao wakiwa wamefungwa. Kisa ni uchimbaji haramu wa madini. Habari za madini ziliwatia hofu wake wa Luzolo na Mpepo hasa mama Tabu ambaye alikwishadokezewa kuhusu safari ya kutafuta mali. Hapohapo walikuwapo wengine ambao hata waliamini kuwa walikuwa wamechukuliwa na majini au mashetani. Mradi mambo yalikuwa ya wasiwasi, waliokwenda kwa mganga walikwenda, walioamini mizimu nao walitambika na kadhalika.

Nini kiliendelea baada ya kufkishwa kituo cha polisi?

Tuendelee mwezi ujao.

# ELIMU JAMII

## HAKUNA MWANAFUNZI ANAYEPENDA KUFELI

HAKUNA MWANAFUNZI ANAYEPENDA KUFELI (Marudio)

Makala haya ni maalum kabisa kwa wazazi na walezi wote wenye wanafunzi mwaka 2024

Moja ya vitu ninavyoviamini ni kuwa hakuna mwanafunzi anayependa kufeli,hakuna mwanafunzi anayetamani kumaliza shule na kukosa cheti. Kufeli ni matokeo ya changamoto nyingi anazokutana nazo mwanafunzi katika safari yake ya kufuta ujinga. Ambatana nami katika kuangalia changamoto hizo kwa uchache wake;

Usimamizi hafifu,shuleni kuna wanafunzi wachache sana ambao wanahitaji usimamizi mdogo,walio wengi wanahitaji usimamizi wa karibu sana, mzazi ukimsahau mwanao hata siku mbili jua kuwa umepoteza pakubwa saana. Ikitokea mzazi katingwa,mwalimu naye kazidiwa na majukumu,kwa pamoja wameshindwa kabisa kumsimamia mwanafunzi tambua kuwa mwanafunzi husika hawezi kufanya vizuri kamwe. Mzazi jukumu lake ni dogo lakini linamchango mkubwa sana kwa mwanafunzi. Mzazi inakupasa kutumia dakika kumi ama kumi na tano kumsikiliza mwanao yale aliyojifunza siku hiyo,kumsisitiza kusoma na kuonesha kuwa unamfuatilia. hii ikifanyika kwa mwendelezo basi kufaulu inawezekana.

Marafiki wabaya,mwanzoni nilikuwa sielewi ni kivipi marafiki wanaweza kuwa chanzo cha wanafunzi kufeli. Ila kwa sasa ninaamini kuwa urafiki mbaya unapelekea wanafunzi kutokufanya vizuri. Les brown anatolea ufafanuzi zaidi juu ya madhara yaliopo kwenye urafiki usio na tija kwa mfano wa nyanya nzima na nyanya mbovu anasema ukiwa na nyanya nzima tano na mbovu moja zikiwekwa sehemu moja yaani kwenye chombo kimoja kwa siku tatu nyanya nzima zilizokuwa karibu na ile mbovu moja zitaanza kuharibika,ndivyo hata kwenye kufaulu,mwanafunzi akiambatana na wanafunzi wenye tabia zisizopendeza na wao wanaathirika kama ilivyo kwenye nyanya.

Tabia mbaya, hapa namaanisha tabia zote ambazo zinakinzana na utaratibu wa maisha wa kila siku na zile zinazokinzana na maadili ya uanafunzi. kinacholeta ufaulu mzuri ni tabia. Subira ni mwanafunzi wa kidato cha nne anayefanya vizuri sana darasani ilipofika mwezi wa sita baada ya mtihani wa mock alianza visa na vitimbwi. Kila siku alikuwa anapewa adhabu,basi hekaheka zilienda mpaka mwezi wa nane. Kufika mwezi wa tisa akastuka,akawa mpole akashuka chini,akatulia na kuanza kusoma,alisomasoma na mwisho wa siku aliishia kupata daraja la tatu badala ya daraja la kwanza zuri. Mzazi kamata nidhamu ya mwanao shirikiana vizuri na walimu wake.

Mambo mengi,mwanafunzi mwenye mambo mengi ni ngumu kufanya vizuri katika masomo yake watu wengi husema ili mwanafunzi afaulu ni lazima afeli kwanza mambo ambayo hayana faida katika safari yake ndipo afanye vizuri darasani.

Kukosa ratiba,kingine kinachomfanya mwanafunzi kutokufanya vizuri ni kukosa ratiba. Ratiba ndio uti wa mgongo wa wanafunzi, Mwanafunzi asiye na ratiba binafsi anaweza akawa anasoma somo moja ama mawili kwa wiki ama mwezi mzima na kushindwa kusoma masomo

mengine.

Kukosa mwendelezo,ili mwanafunzi aweze kushika na kuhifadhi alichokisoma anapaswa kuwa na mwendelezo wa kujisomea kila wakati.

Kutokujijua,ipo namna hii mwanafunzi asiyejua ni njia ipi inawezakumsaidia kuelewa hataweza kufanya vizuri.

Kutokufanya maswali mengi,tunaishi katika ulimwengu ambao unabadilika kila siku,zamani maswali yalikuwa  ya moja kwa moja kiasi kwamba mwanafunzi akikomaa na notes anauwezo wa kufanya vizuri lakini sasa hivi bila kutafuta maswali ni ngumu sana kumudu kujibu maswali kwenye mtihani, usomaji uendane na ujibuji wa maswali.

Mazingira,mazingira chanya huleta matokeo chanya, mwanafunzi akikosa mazingira mazuri ya kujisomea uwezekano wa kufanya vizuri  unakuwa mdogo,wazazi jitahidini kuwapatia watoto wenu mazingira tulivu ya kujisomea.

Uvivu,wanafunzi wengi wanafeli kwa sababu ya uvivu wengi wao hawapendi kujisomea. Namkumbuka mwanafunzi wangu mmoja tumwite Halima aisee alikuwa anapenda sana kusoma siku ya mahafali  yake alipokea zawadi kwenye masomo yote,na cha ajabu kesho yake asubuhi sana alikutwa darasani akiendelea  kujisomea wakati wahitimu wenzake wakiwa wamelala na kufurahia zawadi walizoletewa.

Kukosa ramani ya anakokwenda,wanafunzi walio wengi wanasoma ama wanaenda shule wakiwa hawajui sababu ya kwenda shule. Wengi wanakwenda shule kwa sababu wamefaulu hawajui kabisa faida ya kusoma wala ya kufaulu,hii inawafanya wasijisomee.

Kutokujua asome nini ili awe nani,hii changamoto sijui niirushe kwa wazazi,wanafunzi ama walimu. Kwakuwa kuna msemo usemao elimu huanzia nyumbani naomba tu niirudishe kwa mzazi, mzazi unajukumu la kumsadia mwanao kufahamu asome nini ili awe nani hii itapunguza wimbi la wanafunzi wanaojiita madaktari na hawasomi fizikia na kemia.

Kutokutimiziwa mahitaji,moja ya sababu inayowafanya wanafunzi kutokufanya vizuri ni ukosefu wa mahitaji mathalani madaftari,kalamu na mahitaji mengine muhimu. Namkumbuka mwanafunzi wangu mmoja anamadaftari manne ilhali anamasomo saba. Anachokifanya sasa daftari moja anaandika masomo mawili kimbembe huja muda wa kufanya maswali marazote hushindwa kukusanya madaftari hayo kwa hofu ya kupewa adhabu.

Kukosa msimamo,Msimamo ni muhimu sana kwa kila mwanadamu lakini zaidi sana kwa kila mwanafunzi,tuliopo mashuleni tunaona jinsi gani mwanafunzi asiye na msimamo anavyopelekwa/pelekeshwa na wenzake. Mwanafunzi asiye na msimamo maranyingi sana huamuliwa mambo mengi na wenzake. Hasa maswala ya kusoma.

Usiache kunifuatilia facebook na instagram

JULIANA ISONDO

Soni Day Sekondari

Bumbuli Tanzania

0758463395

# HAPPY NEW YEAR—Twahir Yusuph

Nchi nzima ilisimama, kila kituo cha habari ililizungumzia tukio hilo tu. Viongozi wa serikali ngazi za ulinzi walipigwa butwaa, machapisho ya raia yalipishana mitandaoni. Taharuki ilikuwa kubwa, kila mmoja akiwa na simulizi ya tukio hilohilo kwa namna alivyolipokea.

"Yaani anarekodi kabisa anavyomuua mtu, kisha anapost mtandaoni!" komenti ya mchangizi mmoja iliakisi mshangao.

"Achana kumuua na kumpost, tena jamaa alivyokatili akamsindikiza na Caption ya Happy new year, halafu kaiandika kwa herufi kubwa, Aisee Dunia simama nishuke."

Yalikuwa majadiliano ya baadhi ya raia mtandaoni, wakilizungumzia tukio hilo walililoliona. Iliwastaajabisha wengi, swali gumu ambalo hata polisi walishindwa kulitatua, ni kwanini mtu huyo arekodi mauaji kisha ayaoneshe hadharani? Haogopi sheria? Lakini kwanini pia ajifiche! Yaani aonekane kivuli tu kwenye video hiyo chafu na isiyofaa kutazamwa hata hiyo mara moja yenyewe?

Tena kupitia kurasa yake yenye jina moja tu, KIFO. Analengo lipi? Sababu za kumuua je? Lundo la maswali tata yalivijaa vichwa vya polisi wote, wakuu na wadogo ambao walikuwa mkutanoni saa hiyo. Halikuwa tukio lililozoeleka, vikao vya dharula viliitishwa haraka. Pia ilitangazwa kauli ya kusikitishwa na kitendo hicho kutoka kwa Rais wa nchi hiyo Profesa Omar Kifaranga, ambaye aliliagiza jeshi la polisi limtafute mtu huyo na akamatwe mara moja. Pia Rais hakuishia hapo, alitoa pole kwa mkuu wa jeshi la polisi nchini, ambaye kitendo hicho cha kikatili kilifanyika kwenye roho na mwili wa mwanawe, kijana wake wa kiume. Yaani kauliwa mtoto wa mtu mwenye hadhi kubwa serikalini, kisha muuaji akataka Dunia nzima ishuhudie. Kwanini?

"Nasema hivi, nataka hii kazi ifanyike ndani ya saa 48 huyu mtu awe tayari mikononi mwetu." Sauti iliyoakisi kutokuwa na mzaha ilipaza kwenye chumba hicho cha mkutano, ikikitoka kinywa cha Mkuu wa jeshi la askari polisi, aliyezibeba mboni zilizokoza rangi nyekundu kwa hasira. Hakuna aliyebisha, ni mbele ya kikao cha ghafla, kilichosababishwa na kifo cha maajabu ndani ya Taifa lao, kifo ambacho aliyekifanya alikuwa anafurahia huku wao wanaona, sio wao ni Taifa zima limekishuhudia. Ni kifo cha fedheha, alichofanyiwa mwanawe yeye kiongozi wa jeshi la kulinda usalama wa kila raia na mali zake, ina maana muuaji hakutambua hilo?

Askari wote walitii, kikao kikafungwa rasmi, huku operesheni ya kumsaka katili huyo, mtu mwenye roho mbovu zaidi isiyoshoneka, mlango wake ukifunguliwa. Askari waliianza kazi yao usiku huohuo, wataalamu wa kimitandao wakapewa jukumu la kwanza, la kumfichua mmliki wa akaunti yenye jina la KIFO iliyotandaza video hiyo chafu. La pili ilikuwa kuichunguza video ile kiyakinifu, kama wataweza kupata chochote cha ushahidi, kitachowafanya wamshike muuaji huyo ambaye alikosa hata stara ya kuitoa roho ya binadamu mwenzie kisirisiri.

Nchi ilizizima, mitandaoni hapakuwa na hadithi tofauti, licha siku hiyo pia timu shindani za Taifa lao zilicheza japo hazikufungana. Mitaani palilakiwa na ukimya. Edward Kituo, mkuu wa jeshi la polisi, baada ya kikao kile cha dharula kutamatika, akiwa bado ndani ya chumba hicho amejiinamia, habari nyingine za kushtukiza zinawasili, hizi anapewa na askari aliyesimama mbele yake akitweta, ambaye aliingia bila hodi chumbani humo.

"Nini?" alifoka, akimtazama kwa macho makali afande huyo. Labda kwa mdomo aliona atamchelewesha, afande huyo mwenye cheo cha chini, aliitoa simu yake na kumwekea mbele ya uso wake aone, ni mbele ya mboni za IGP Edward Kituo zenye afya. Pigo lingine kwa Edward Kituo, muuaji amechapisha kipande kingine cha video, inayoonesha eneo ambalo ameuacha mwili aliousasambua kikatili, huku akiacha maelezo wasisumbuke,

*"BEACH YA GYM KHANA, NJOENI MUUCHUKUE MZIGO WENU MKAUZIKE, MI MSTAARABU SANA JAMANI, NA MWEMA MNO."*

Hili hakulivumilia Edward. Mbio akielekea nje ya makao hayo makuu ya polisi, askari wote tayari walikuwa na taarifa hizo. Akazama garini mwake haraka haraka, hata dereva wake hakuuliza, alitambua ni wapi anapopaswa kuelekea, naye alikuwa askari polisi pia. Ndani ya gari, akiwa ameketi siti ya nyuma, macho yake yalitiririsha machozi, ule ukakamavu aliojigamba nao kikaoni muda mchache uliopita, nyakati hii ulimuomba mapumziko. Viganja vyake vilivyoijenga ngumi vilikuwa juu ya kinywa chake alichokifunga, huku akiweka kiwiko cha mkono wake dirishani kwenye kioo, amechanganyikiwa. Mwili wake ulistarehe ndani ya gari, mawazo yalimwonesha picha nyingi za mwanae akiwa hai, tena na tabasamu alilozoea kumuona nalo.

Hiyo ilizidi kumuumiza na kumtesa. Akafaulu kukizuia kilio cha sauti, ila machozi na majonzi yaliyoshindwa kujificha usoni pake vilimuumbua, alilia Edward. Kadri matairi ya gari yalivyozidi kumsogeza alipolala mwanawe kipenzi asiye na roho wakati huo, uchungu nao ukaacha kumlindia sauti yake, aliipaza akilia kwa kugugumia.

"Amekufanya niii..niii" taratibu sana, tena kinyonge mno huku akishikwa na kigugumizi alisononeka, ilhali mboni zake zikiendelea kuiachia mvua ya machozi kistaarabu kabisa. Ni kama alikuwa akimuuliza muuaji ambaye kana kwamba anamuona. Wote huo ulikuwa uchungu unaopenya kwenye hisia zake kwa fujo, hisia alizoshindwa kukabiliana nazo. Hapakuwa mbali, ni chini ya dakika tano tu ndizo walizopoteza wakiwa barabarani, sasa walifika kwenye fukwe hiyo waliyoelekezwa kuachwa kwa mwili huo, ni hapohapo Posta, eneo la GYM KHANA, ndani ya jiji lao la SENI.


Katikati ya barabara, karibu kabisa na bahari, kiroba kilicho na maiti ya mwanawe kiliachwa kweli, ni mtoto wake ambaye kilitengwa kila kiungo cha mwili wake. Aliteremka kwenye gari yake macho yakiziba kwa ukungu wa kilio kilichomsulubu garini, haraka akatembea hadi mbele ya kiroba hicho huku askari wengine wakimfuata. Huzuni ikiwa imemchosha, miguu ikimtetemeka mkuu wa polisi wote nchini, huku machozi yakizitapakaa mboni zake zinazokitazama kiroba ambacho kina vipande vya mwili wa mwanawe.

Pembezoni mwake kuliwekwa sanduku la wastani, alilisogelea Edward, taratibu akalifungua huku akitetemeka.

Hakuamini, yowe la kuugulia lilikichopoka kinywa chake, humo ndimo kilipohifadhiwa kichwa cha mwanawe, alikiona. Hiyo ilimuumiza kuliko huzuni zote alizowahi kukutana nazo ulimwenguni. Alilia kama mtoto IGP Edward Kituo, nguvu zilimwisha miguuni, akadondoka na kuilalia sakafu ya barabara hiyo ya lami akimwaga machozi ya uchungu kuliko binadamu yeyote aliyewahi labda. Ilikuwa siku mbaya, mbovu, na iliyomtisha mno tangu azaliwe. Nini angefanya zaidi ya kuyatumia machozi kitengo hicho inachokipendelea? Laiti kungelikuwa na duka la kuuza uhai, labda angeliununua mpya kwa gharama yoyote ile, ili amrejeshee mwanawe aliyefanywa kama kitoweo buchani.

Aliteseka, lami ya barabara hiyo ililowana kwa machozi yake yenye maumivu makali yasiyovumilika. Punde waandishi wa habari walionekana kufika eneo la tukio, lakini askari walizizuia kamera zao zisichukue chochote kilichokuwa kinaendelea nyakati hiyo. Magari ya askari polisi yaliongezeka, jumla yakawa matano. Maafande wakalivaa jukumu la kumtuliza kiongozi wao, walimwinua na kumpakiza garini.

***Itaendelea toleo lijalo...***



# "SHEMEJI USIZIME TAA…! NAOGOPA UKIMWI…! - 02

Na. G.K. Jr. Rogger Miller

**"Sawa ni kweli bado mapema na kuna watu wengi. Lakini uwingi siyo tija. Kuna wema na wabaya. Shaka yangu ni huu mzigo nilionao" alisema na nikamuona kabeba boksi la wastani. Maandishi yake yalionesha kuwa kulikuwamo ndani ya boksi "deck" ya video (VCR) aina ya Sony.**

***Endelea…***

Nikatingisha kichwa kukubaliana naye na nikataka kumwambia akodi taksi, lakini moyo ukasita. Kwakuwa ile ilikuwa tripu yangu ya mwisho, niliingiwa na huruma na kuona bora nimpeleke. Kwani kutoka Muleba kwenda Loyola hapakuwa mbali, na pia kumsaidia binti kama huyu 'late' time kama hizi ningeweza kubwabwaja upuuzi wa hapa na pale, ambao unaweza kuniunganisha naye kwenye fani fulani.

Kabla sijafikia muafaka wa kuitekeleza huruma yangu, nilimwita 'konda' wangu tukateta kidogo.

"Haya anti, njoo uingie na uketi huku mbele tukusidikize, isitohe ni usiku saa hizi, ili iwe rahisi kunielekeza," niliongea kwa upole, lakini nia yangu ilikuwa ni kuwa karibu naye ili niweze kuongea naye kwa urahisi.

"Asante, utakuwa umenisaidia sana Anko" alisema na kuja mbele ya gari hili aina ya Toyota Hiace nililokuwa naendesha.

"Usijali, lakini ni kwa ajili yako na kwa usalama wako, hii siyo 'route' yetu" nilisema ili athamini zaidi msaada wetu.

"Asante," alizidi kushukuru huku akijiweka vyema kwenye 'seat'. Macho yangu yasiyokuwa na pazia, yalishuhudia mapaja manene yaliyonona, nikahisi kupandwa na mzuka wa kwetu, nikameza mate. Kabla macho yangu hayajafaidi vyema aliivuta sketi yake kuyafunika, lakini haikufua dafu. Alipoona sketi haimsaidii alichukua boksi lenye mzigo wake, alipakatia na kuyaficha kabisa maungo yake.

"Hongera sana Anti, yani ukapa wote huu umeibua deck ya Sony" nilimchokoza.

"Asante, lakini siyo yangu, nia ya mjomba wangu ninayekaa kwake, aliniagiza. Miye jeuri ya kununua deck sina, kwani hata kazi sijui nitaanza kufanya lini, kwani bado nipo masomoni" alinifafanulia, nikatamani kuzidi kumdodosa.

"Okay, wewe nawe ongeza bidii masomoni kuna siku utakuja kufanya mambo kama haya" nilimjibu huku nikitumbukiza gia na kuzungusha usukani kwa uhodari. Gari likaserereka kwa kasi kuelekea Mabibo Farasi. Macho yangu hayakuzubaa na nililisanifu umbo lake kiwizi na kugundua alikuwa mtoto 'bomba' si mchezo. Sura yake ilikuwa pana yenye macho ya kuita, pua ya kimeru na midomo mitamu iliyosheheni vyema juu ya kidevu kilichochongoka kama pembe au ncha ya Kusini ya Bara la Afrika. Shingo ya kunyirizika kama….

Ilibidi nistuke na kuiweka gari sawasawa barabarani, kwani uzuri wa binti yule ulishaanza kuniehusha na kusahau jukumu langu. Nikapunguza spidi na kurekebisha sauti ya redio, na kutyuni Redio Free Afrika na kukutana na KiD BOY alirusha hewani salamu za wapendanao kutoka jijini 'Ng'wanza'. Nikaacha hapo na kuendelea kuendesha gari huku nikimsanifu binti yule kwa chati.

Shingo yake ilichomoza toka kwenye kifua maridhawa kilichopambwa na embe dodo changa ambazo zilionesha ujana wake. Zilitulia 'kishari' ndani ya blauzi yake, kama mizinga ya kutungulia ndege. Na laity ncha yake ingekuwa kali zingeitoboa blauzi, nikameza mate. Nikaweka miadi ya kuzinyonya siku fulani, Mungu akipenda (Inshallah).

"Sijui waitwa nani Anti?"

"Naitwa Rehema, lakini hupendelea kuitwa Ray"

"Uliniambia uko masomoni, wasoma wapi?"

"Niko Chuo cha Elimu ya Biashara, ninachukua kozi ya Uhasibu"

"Vyema, ongeza bidii, tunahitaji wahasibu wengi sana nchi hii" nilimchombezea.

"Inawezekana, niombee kwa Mungu nifaulu vizuri. Lakini dereva, hujaniambia jina lako" alisema huku amenikazia macho, kwa bahati macho yetu yakagongana. Yake yalikuwa mang'avu, nikahisi yaliona mpaka ndani ya mawazo yangu.

"Naitwa Donald Kwambiji, au Don kwa ufupi lakini wengi huniita D.K"

# HADITHI

“Don K, au D.K ni jina zuri kweli”

“Asante, lakini halishindi la kwako, Ray ni jina zuri na mara nyingi, au akina Ray wenghi ninaowafahamu ni wazuri katika fani zote” nilisema kumchanganya na kumleta kwenye anga zangu.

“Akha! Hayo ya kwako wewe tu” alimaka, kisha akaendelea kulonga. “Isitoshe inaonekana mambo yako siyo mabaya. Inaelekea hii gari ni yako maana nimeona tiketi zake zimeandikwa DK. TECHNICS, hongera sana” alisema huku akitabasamu, nikagundua mpangilio wa meno yake ulikuwa na kombora linguine ‘kunimong’onyoa’ mtima wangu. Hatari! “Hapana Ray, hii ni gari ya familia, siyo yangu peke yangu, D.K. Technics ni kampuni” nilijibaraguza, ingawa kweli alikuwa amegonga, kwani gari hii ni yangu na D.K. Technics ni kampuni niliyoaianzisha mwenyewe. Akaendelea kutazama tiketi ambayo ndiyo iliyomfanya agundue hilo.

Wakati huu Dj Sandu au Kidboy alikuwa akiongea na watu waliokuwa wakipiga simu kuwasalimia wapenzi wao. Niligundua Ray aalifurahia kuwasikiliza, nikamtupia swali katika kutafauta njia ya kumwingiza kwenye anga zangu. Sikuwa nimekosea kwani alikuwa karibu mno na kipindi kile.

“Ray, unaonekana kufurahia kipindi hicho”

“Of Course, yani kumtakia njozi njema yule umpendaye ni Jmbo zuri, linafurahisha, wewe hupendi?”

“Hapana! Ninapenda, tatizo huyo nimpendaaye hajapatikana” nilijitetea huku macho nimeyakaza barabarani, nikiendesha kwa uangalifu. Nikamsikia akiguna, kisha akasema, “usiniongopee D.K kama ni kweli hayupo mtafute utampata”

“Kweli,d lakini ingekuwa poa sana kama huyo mtu angekuwa ni wewe” nilisema moja kwa moja kukiri udhaifu wangu na nikatarajia jibu lolote baya. Kwani ‘wasomi’ nawajua wasivyowamaindi madereva daladala. Hakunijibu, badala yake aliniangalia kwa jicho kali, nikahisi amechukia.

“Samahani kama nimekuudhi, kwa kukuchagua, lakini huo ndio ukweli wenyewe… niko mpweke na ninahitaji mwenzi”

“No! Just a matter of time, una haki ya ‘kumuaproach’ binti yeyote. Kwa upande wangu sina chochote cha kukuambia, labda hapo baadae, tukijaliwa kuonana miaka ijayo”

Jibu lake lilinimaliza nguvu na nikahisi amechukia….

***Itaendelea toleo lijalo...***

ANAANDIKA ANNA MELEIYA MBISE

Kusoma vitabu kudumu!

Nilikuwa Bukoba kwenye harakati na niliweza kuonana na msomaji David Ernest ambaye kwakweli alinielezea namna ambavyo usomaji umemsaidia kusimamia miradi yake ya maendeleo kikamilifu.

Alinipatia zawadi zitokanazo na kazi zake, kwa kweli ilikuwa ni furaha. Tunahitaji kutumia maarifa kuzalisha bidhaa na kuwa watu bora.

Maarifa ni mtaji na tuyatumie kuwajenga wengine.





**Pichani juu: Ndizi mbivu kutoka kwa David. Chini: Anna Mbise na David Ernest**

**Tangazo**




# MSALITI

## Jipatie nakala yako kwa Tsh

## 15,000

- Kona ya Riwaya KINONDONI - 0655428085
- Posta Mpya kwa George



Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com